SportPesa
TZS. 823,998,440
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Binti**, waganga wa jadi mbaroni tuhuma kumuua mama

UKURASA 3



**MOURINHO ASHANGAA KICHAPO**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumanne Januari 11, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579822

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Samia: Sijawaacha

● **Afichua** siri Lukuvi, Kabudi kutokuwa kwenye Baraza... *Endelea ukurasa 2*



Aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wiliam Lukuvi (kulia), akizungumza na baadhi ya mawaziri baada ya kuapishwa jana, Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma. Kutoka kushoto ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi na Ajira, Prof. Joyce Ndalichako. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Vielelezo kesi dhidi ya Mbowe vyagonga mwamba

UKURASA 4

## Tulia ajitosa mbio U-spika

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA NA 'SAPRAIZI' BAB'KUBWA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# SAMIA: SIJAWAACHA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amefichua sababu za kuwaacha katika Baraza la Mawaziri aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi na aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi kuwa lengo lake ni kuwatumia kuwasimamia wengine.

Pia amemaliza minong'ono iliyoanza kutawala kuwa Lukuvi ameachwa kwenye baraza hilo alilolitangaza Jumamosi iliyopita ili agombee nafasi ya Spika kuwa wasimzushie kwa kuwa hatagombea nafasi hiyo.

Akizungumza katika hotuba yake fupi iliyochukua dakika nne na sekunde 25 baada ya kuwaapisha mawaziri, manaibu mawaziri na makatibu wakuu jana Ikulu ya Chamwino, alisema: "Nataka niseme jambo moja tu nina kaka zangu wawili Lukuvi na Kabudi ukiwatizama hawa 'age' (umri) yao kama yangu na ukiwatizama niliowateua hamfanani kabisa kwa hiyo kaka zangu wawili hawa nimewaleta waje kwangu ili waje wanisaidie kuwasimamia nyie.

"Kwa hiyo kuwaacha kwangu kwenye hii 'list' (orodha) ni kwa sababu hapo wote wadogo na mnahitaji kusimamiwa vizuri, hivyo hawa wawili watakuja kwangu ili tuwasimamie nyie vizuri," alisema Rais Samia.

Akimzungumzia Profesa Kabudi, alisema kutokana na kufanya kazi nzuri ya kusimamia mazungumzo ya serikali na mashirika ameamua kumpa eneo hilo kulisimamia ipasavyo.

"Lakini jingine kaka yangu Kabudi amefanya kazi nzuri sana kusimamia mazungumzo ya serikali na mashirika na ndiyo kazi ambayo nataka nimkabidhi sasa aifanye kindaki ndaki aendelee na kazi hiyo, ila kwasababu kazi yake haipo kwenye muundo haitangazwi wala nini, lakini atasimamia hiyo kazi mashirika yote kazi zote zitakazoingia ubia na serikali Kabudi ataongoza hiyo timu kwa hiyo yeye ni baba mikataba," alisema.

"Kaka yangu Lukuvi yeye ana kazi na mimi, mtaisikia baadaye lakini nawavuta Ikulu kazi yetu ni kuwasimamia nyinyi kwasababu mkiwatizama hapo wote wanakaribia kustaafu bado miaka miwili wengine bado mnasafari ndefu kwa hiyo kazi yetu ni kuwasimamia nyie pamoja na makatibu wakuu," alisisitiza Rais Samia. Alisema kutokana na hali hiyo, Lukuvi bado yupo hajatoka kama ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakifurahia kuachwa kwenye Baraza la Mawaziri.

"Kuna watu nawasikia wanasema afadhali Lukuvi katoka, hajatoka yupo na wengine wameanza kumletea ujumbe mfupi za ajabu ajabu wakijua atagombania uspika hatagombea ana kazi na mimi kwa hiyo hatokuwa Spika na wala hatogombea uspika msianze kumchafua, ametumikia taifa hili kwa uadilifu na muda mrefu mwacheni aende na mimi," alisema. Kwa upande wake Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema atakaa pamoja na mawaziri waliochaguliwa kupeana majukumu mbalimbali pamoja na kuyafanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa na Rais.

"Mheshimiwa Rais tunaahidi kuendelea kufanya kazi kwa uaminfu, uadilifu mara nyingi umekuwa ukisisitiza kufanya kazi kwa matokeo chanya tunakuhakikishia kuwa tutafanyakazi kwa matokeo chanya ili kuwafikia wananchi hadi kule chini," alisema. Awali, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema Bunge lipo tayari kushirikiana na kuyafanyia kazi mambo yote yatakayoletwa na mkuu huyo wa nchi.

"Naomba nitoe ufafanuzi hapa kuwa wewe ndiye mkuu wa nchi ambaye nafasi yako huwezi kuilinganisha na kiongozi yeyote wa muhimili mwingine, hivyo mheshimiwa Rais sisi kama Bunge tutakuwa tayari wakati wote kufanya kazi ambazo utahitaji kushirikiana nasi," alisema Dk. Tulia.



Rais Samia Suluhu Hassan, akimwapisha Pindi Chana kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. PICHA: IKULU

## Majaliwa aomba mataifa kushirikiana nchi za Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye Jukwaa la Nne la Vijana Duniani lililoanza jijini Sharm-El-Sheikh, Misri.

Akishiriki mkutano huo kwa njia ya mtandao kutoka ofisini kwake Mlimwa, jijini Dodoma, Waziri Mkuu ameyaomba mataifa makubwa duniani yashirikiane na nchi za Afrika ikiwamo Tanzania ili kuhakikisha uchumi wa nchi hizo unarejea katika hali yake ya kawaida kutokana na madhara ya UVIKO-19.

"Tangu kuingia kwa wimbi la kwanza la UVIKO-19, tumeshuhudia athari kubwa za kiuchumi na hasa kwa vijana. Vijana wamekuwa wakichangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu, lakini uwepo wa UVIKO-19 umeathiri maendeleo ya sekta ya utalii ambapo vijana wengi wameajiriwa."

Ameongeza kuwa UVIKO-19 umeathiri uwekezaji katika viwanda na kwenye sekta ya miundombinu ambako kampuni nyingi zilitoa ajira kwa vijana, lakini hazikuweza kufanya kazi na kuleta athari kubwa.

Akitoa mfano, alisema Rais Samia alipata fursa ya kuzungumza katika mkutano wa Umoja wa Mataifa uliofanyika Marekani mwaka jana na kueleza athari za ugonjwa wa UVIKO-19 na Tanzania ikapata mkopo nafuu uliotumika kujenga madarasa na vituo vya afya kama njia ya kurejesha uchumi.

"Tumehamasisha Umoja wa Afrika (AU), uchukue suala hili kama ajenda ili uweze kujadili namna bora ya kurejesha uchumi wa Afrika; Tanzania ikiwa mwanachama wa AU nayo pia itaingia kwenye mjadala huu na tutapata njia bora ya kurejesha uchumi wetu hasa tunapolikabili wimbi la nne."

Alisema Tanzania imeonyesha inahitaji kuungwa mkono katika jitihada zinazochukuliwa kwenye ujenzi wa miundombinu ili Watanzania na hasa vijana waweze kushiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na uchumi wa jumla wa kitaifa.

Viongozi wengine walioshiriki mkutano huo ni Rais wa Misri, Abdel Fattah Al-Sisi, Rais wa Colombia, Ivan Derque Marques, Rais wa Romania, Klaus Iohannis, Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, Rais wa Malta, Malta George Vella na Waziri wa Nchi wa Falme za Kiarabu anayeshughulikia Masuala ya Vijana, Shamma al Mazrui.

Mkutano huo wa siku nne ambao unashirikisha wajumbe zaidi ya 5,000 kutoka nchi mbalimbali duniani, unalenga kujadili madhara ya UVIKO-19 kwa vijana na namna gani nchi zimeweka mikakati ya kukabiliana nazo katika shughuli za kiuchumi, mabadiliko ya tabia nchi, hifadhi za jamii, haki za binadamu na uhifadhi wa mazingira.

# Wanachama tisa wajitosa kugombea U-spika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANACHAMA tisa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamejitosa kuchukua fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea nafasi ya Spika wa Bunge, akiwamo Naibu Spika, Dk. Tulia Akson.

Dk. Tulia pia ametoa ufafanuzi kuhusu nia yake ya kugombea nafasi hiyo ya juu katika muhimili huo.

Alisema amechukua fomu ya kugombea nafasi hiyo kwa kuwa Katiba inamruhusu na kwamba anayo haki ya kugombea katika nafasi hiyo.

"Labda niweke sawa nimegombea nafasi hii kwa kuwa Katiba inaniruhusu mimi kama Naibu Spika naweza kugombea nafasi hii ya uspika, Katiba imewabana mawaziri pamoja na manaibu mawaziri ndiyo hawaruhusiwi kugombea katika nafasi hii," alifafanua Dk. Tulia.

Akizungumzia nia yake ya kugombea nafasi hiyo, Dk. Tulia, alisema kama atapa nafasi ya kuwa Spika wa Bunge atatoa ushirikiano kwa wabunge ili kuisimamia serikali, kuikosoa na pia kufanya nayo kazi.

Naye Mbunge wa Mlimba, Godwin Kunambi, akiwa mmoja wa wanao wania nafasi hiyo alisema kuwa anataka kutumia nafasi hiyo kuliendesha Bunge kwa misingi ya usawa, kanuni na sheria bila kujali itikadi za vyama, rangi au kabila.

Alisema ana uzoefu wa kuongoza na kutokana na taaluma yake ya sheria, ataliongoza Bunge kwa viwango vya juu zaidi.

"Ninaomba ridhaa ya kuwa spika kwa kuwa uwezo wa kuongoza ninao na nina shahada ya sheria, shahada ya pili ya utawala hivyo ninaweza kuongoza bunge kwa kufuata misingi ya Katiba pamoja na kanuni za Bunge.

"Nikipewa ridhaa ya kuwa Spika nitafuata usawa na hakutakuwapo ubaguzi wala upendeleo wa aina yoyote na kila mbunge atapewa haki yake ya kikatiba, kikanuni na kwa kufuata misingi," alisema.

Katibu Mkuu Msaidizi Idara ya Oganaizesheni CCM Taifa, Solomon Tunda, alisema chama hicho kimeanza mchakato wa kutoa fomu za kuomba kuteuliwa kugombea nafasi ya Spika kwa wanachama wake jana.

Tunda, alisema mchakato huo ambao umeanza rasmi jana, unatarajiwa kukamilika Januari 15, mwaka huu na baada ya hapo vitaanza vikao vya ndani kwa ajili ya kuchuja majina ya wagombea nafasi ya uspika kupitia CCM.

"Wanachama walijitokeza kuchukua fomu katika ofisi za makao mkuu ya CCM Dodoma ni sita ambao ni Dk. Simon Ngatunga, Tumsifu Mwasamale, Merkion A. Ndofi, Dk. Tulia Ackson, Godwin Kunambi, pamoja na Abwene Stephen Kajula," alisema.

Vilevile, alisema katika ofisi ndogo ya chama Lumumba, Dar es Salaam waliochukua fomu ni Patrick Lubano Nkandi, Stephen Julius Masele na Hamidu Ubaidi Chamani.

Hata hivyo, alisema hadi zoezi hilo linafungwa kwa siku ya kwanza katika ofisi kuu ya Zanzibar hakuna mwanachama aliyekuwa amechukua fomu.

## HABARI KITAIFA



Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango akiagana na viongozi mbalimbali katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam wakati akiondoka nchini kuelekea Lilongwe nchini Malawi kumwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika mkutano wa dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC) utakaofanyika leo. PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# Binti, waganga kienyeji mbaroni mauaji ya mama

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SIRI nzito kuhusu mpango wa mauaji ya kikatili ya muuguzi mstaafu wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Patricia Ibreck (66) imefichuka, baada ya polisi kuanika chanzo cha kifo chake ni kuhoji matumizi ya Sh. milioni 60 za kiinua mgongo chake.

Muuguzi huyo raia wa Tanzania mwenye asili ya Kijerumani, anadaiwa kuuawa mwezi Februari, mwaka jana na mwanawe wa kike na kisha kumzika kwa kificho pembeni ya nyumba yake ndogo iliyoko Kijiji cha Uru-Mkuruti, Kata ya Uru Kusini, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Simon Maigwa, hadi kufikia jana mchana, watu watatu walikuwa wakishikiliwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano kuhusiana na mauaji hayo.

"Kati ya tuliowakamata wakihusishwa na mauaji haya, yumo mtoto wa kike wa marehemu pamoja na waganga wawili wa kienyeji. Kati yao mganga mmoja anatokea Mkoa wa Tanga na mwingine jijini Dar es Salaam.

"Uchunguzi wetu wa awali unaonyesha kuwa waganga hao, walikwenda nyumbani kwa marehemu kwa ajili ya kumpatia tiba mama huyo aliyekuwa mgonjwa. Sasa wakati akiendelea kupatiwa matibabu ya asili, mama huyo alishtukia zaidi ya shilingi milioni 60 za kiinua mgongo alizokuwa nazo zilishatumika na haoni matumaini ya kupona."

Aidha, Kamanda Maigwa alisema, baada ya mama kuhoji matumizi ya fedha hizo, mwanawe wa kike na waganga hao walikuwa wakimtaka Patricia aende akatoe pesa nyingine na kuzuka purukushani iliyosababisha watuhumiwa hao kuamua kutekeleza mauaji yake.

"Walipomaliza kutekeleza mauaji hayo, waliuchukua mwili wake na kuuhifadhi katika moja ya chumba nyumbani kwa marehemu, wakisubiri giza lingie ili wakachimbe kaburi na kuuzika mwili huo," alisema.

NDUGU WAHOFU

Kamanda Maigwa, alisema baada ya watuhumiwa kutekeleza dhamira ovu, baadhi ya ndugu, jamaa na marafiki, walianza kupata shaka ya mwenendo wa mtoto wa kike wa marehemu (hakumtaja jina), kuuza rasilimali, huku mama yake akiwa hajulikani alipo.

Katika taarifa yake, Kamanda alisema binti huyo alianza kuuza mali za mama yake na alipokuwa akiulizwa, alikuwa akijibu anauza ili atume fedha nchini India, ambako mama yake alikuwa akipatiwa matibabu.

Maigwa alifanua: "Desemba 20, mwaka jana, majirani zake walikuja Polisi kutoa taarifa za shaka kwamba huenda Patricia aliuawa miezi 10 iliyopita. Tulianza uchunguzi ikiwamo kukusanya vielelezo na tulifanikiwa kuwatia mbaroni watuhumiwa hao ambao walienda kuonyesha walipouficha mwili wa marehemu.

"Ilipofika Januari 9, mwaka huu, tulifanikiwa kuufukua mwili huo na ndani ya kaburi hilo kulikuwa na panga lenye nywele. Baada ya kujiridhisha kwamba ni mwili wa binadamu ulizikwa bila kufuata taratibu, tulichukua mabaki ya mwili huo na kwenda kuyahifadhi katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Rufani ya KCMC, kusubiri uchunguzi wa kina wa kitabibu," alisema.

Kamanda Maigwa, alisema baada ya uchunguzi wa kina kutoka kwa wataalamu, watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kujibu shtaka linalowakabili la mauaji ya kukusudia.

Jana, Nipashe ilifika nyumbani kwa marehemu Patricia na kuwakuta baadhi ya majirani akiwamo Richard Estomii, ambaye alisema enzi za uhai wake Patricia alijaliwa kuzaa watoto wawili mapacha, mmoja akiwa nje ya nchi na mwingine anayetuhumiwa kumuua mama yake.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Musa Lyari, alisema licha ya kutafuta ukweli kwa muda mrefu, binti huyo hakuwahi kuwaonyesha ushirikiano wa alipo mama yake, zaidi ya kudanganya yuko nchini India akipatiwa matibabu.

"Nimemuuliza zaidi ya mara tano kila anapouza viwanja, kila mara anasema anafanya hivyo ili aweze kupata fedha za matibabu kwa ajili ya mama yake aliyeko India," alisema Lyari.


AgResults INNOVATION IN RESEARCH AND DELIVERY

LAND O'LAKES VENTURE37

**Wito wa maombi ya kushiriki katika shindano la mradi wa AgResults**

**(AgResults Tanzania Dairy Productivity Challenge Project)**

Kwa niaba ya Mradi wa AgResults , Land O' Lakes Venture37 inapenda kukaribisha mashirika na taasisi zinazojihusisha na uuzaji na usambazaji wa pembejeo kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, kushiriki katika shindano la tuzo kwa kutumia mfumo wa kutoa motisha kwa kuuza pembejeo na kutoa huduma za ugani ili kuongeza wigo wa kutumia teknolojia, vifaa na ubunifu kwa ajilli ya kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa kutumia pembejeo zilizo bora. Shindano hili litafanyika katika eneo la Pwani ya Tanzania, hasa Mikoa ya Dar Es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro (bila kushirikisha Wilaya za Kilombero na Ulanga) Land O' Lakes Venture37 inawaalika wote watakaopenda kushiriki katika mradi kutoka kwenye sekta binafsi, taasisi au mashirika ya umma, na taasisi zisizo za kiserikali.

Wito wa Maombi ya Ushiriki (*Request for Application – RFA*) unaeleza historia, malengo, kanuni za kushiriki shindano hili ikijumuisha fomu ya maombi na taratibu za namna kuomba na mawasilisho. Katika kuwasilisha maombi, kampuni / shirika / Taasisi itakubaliana na masharti ya wito wa maombi ya ushiriki, ikiwa ni pamoja na taratibu za maombi na maelekezo yaliyowekwa.

Tafadhali kumbuka muda uliopangwa kwa ajili ya kupokea/kuwasilisha maombi ni saa 11:00 Jioni ya Tarehe 28 Februari 2022. Nyaraka za maombi lazima ziwasilishwe Kwa posta anwani 10517 Dar Es Salaam, kwa kuwasilisha Ofisi za AgResults zilizopo Veterinary Complex;131 Nelson Mandela Road, Dar es Salaam, au zitumwe kwa anwani maalumu ya barua pepe ambayo ni AgResultsTanzania@gmail.com Tafadhali andika **"Competitor RFA-AgResults Tanzania Dairy Productivity Project"** katika mstari wa somo la barua pepe au kwenye bahasha itakayobeba maombi hayo.

Mradi utapitia maombi yote na kutathimini kulingana na vigezo vilivyowekwa. Wale wote watakaofanikiwa kuchaguliwa watajulishwa na kuelezwa namna ya ushiriki.

Ndugu mdau, unahimizwa kuwasilisha maombi kwa wakati ili ujipatie tuzo/motisha na kuchangia maendeleo katika sekta ya maziwa Tanzania. Kama una maswali au maoni tafadhali tuma kwa barua pepe kwa anuani ifuatayo; NMrema@landolakes.com. Tunatanguliza shukrani zetu kwa kwa kutuma maombi ya wito huu kwa wakati na pia tunategemea ushiriki wako katika mradi huu muhimu.

**Pata nakala ya wito wa maombi kupitia:**

**AgResults Tanzania Mradi wa Maziwa - Wito wa Maombi ya Ushiriki Au: :**
**https://agresults.org/news-and-blog/10-blog/227-request-for-applications-for-sales-period-3-competitors-for-the-agresults-tanzania-challenge-project**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**TANGAZO**

Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania anapenda kuwajulisha watu wote wanaotarajia kufanya Mtihani wa **Kidato cha Nne (CSEE)** na **Maarifa** (QT) **Novemba, 2022** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha kawaida cha Usajili kitaanza tarehe **01/01/2022** kwa ada ya Shilingi **50,000/=** kwa wanaojisajili **CSEE** na Shilingi **30,000/=** kwa wanaojisajili **QT** na kitaishia tarehe **28/02/2022.** Aidha, watakaojisajili kwa kuchelewa kuanzia tarehe **01/03/2022** hadi tarehe **31/03/2022** watalipa Shilingi **65,000/=** kwa Watahiniwa wa **Kidato cha Nne** (CSEE) na Shilingi **40,000**/= kwa Watahiniwa wa Mtihani wa **Maarifa** (**QT**) ikiwa ni ada ya kawaida pamoja na faini.
2. Mtahiniwa atakayejisajili kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne **(CSEE) 2022** ni yule ambaye anarudia Mtihani wa **Kidato cha Nne** (CSEE) au amefanya na kufaulu Mtihani wa **Maarifa (QT)** katika kipindi kisichozidi miaka **mitano (5)** iliyopita au mwenye sifa zinazolingana na hizo alizopata kutoka nje ya Nchi na kufanyiwa ulinganifu na Baraza la Mitihani la Tanzania.
3. Mtahiniwa atakayejisajili kufanya Mtihani wa Maarifa ni yule ambaye anatafuta sifa ya kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne kama Mtahiniwa wa Kujitegemea.
4. Usajili unafanyika kwa njia ya mtandao, kwa kufuata hatua zifuatazo;
   (a) Fika Kituo utakachofanyia Mtihani ili kupata namba rejea (Reference Number) ambayo inatolewa bure.
   (b) Fika Ofisi ya Posta kupata 'Control Number' ya kufanyia malipo ya ada ya Mtihani au ingia katika tovuti ya Baraza la Mitihani ili utengeneze 'Control number' ya kufanyia malipo kwa utaratibu ulioelekezwa.
   (c) Fanya malipo ya ada ya Mtihani kupitia Posta au Benki kwa kutumia 'Control Number'.
   (d) Fika Posta kufanya usajili au jisajili mwenyewe kupitia tovuti ya Baraza la Mitihani kwa kufuata hatua zilizooneshwa kwenye tovuti.
   (e) Baada ya usajili kukamilika chapa na wasilisha nakala moja ya fomu Ofisi ya Posta, wasilisha nakala ya pili kwenye Kituo utakachofanyia Mtihani na nakala ya tatu ya fomu itunzwe na wewe (mtahiniwa) mwenyewe kwa ajili ya kumbukumbu.
5. Ufafanuzi kuhusu utaratibu wa hatua za kufuata katika usajili, umetolewa katika tovuti ya Baraza la Mitihani **www.necta.go.tz.** Waombaji wote wanasisitizwa kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa baada ya kipindi cha usajili kumalizika.

**Imetolewa na;**
**KATIBU MTENDAJI**



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akienda kwenye chumba cha Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, kusikiliza tuhuma zinazomkabili. PICHA: JUMANNE JUMA

# Vielelezo kesi dhidi ya Mbowe vyagonga mwamba

**Na Kulwa Mzee**

VIELELEZO vya sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ramani ya vituo vya mafuta na vifaa mbalimbali vya jeshi vilivyokuwa vinatolewa na upande wa Jamhuri katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu, vimegonga mwamba baada ya Mahakama kuvikataa.

Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, ilikataa kupokea kielelezo jana mbele ya Jaji Joackim Tiganga, baada ya kukubaliana na hoja mbili za mawakili wa utetezi za kupinga kupokelewa kwa vielelezo hivyo.

"Mahakama inaona hoja zote zilizotolewa na upande wa utetezi hazina mashiko isipokuwa hoja mbili ambazo Mahakama imezikubali.

"Mahakama imekubaliana na hoja kwamba shahidi hakuwasilisha risiti ya kuonyesha vitu mbalimbali alivyokamata, na alama iliyowekwa kwa utambuzi wa vitu hivyo haikuwa sahihi kwa mujibu wa maelekezo yaliyopo katika mwongozo wa Jeshi la Polisi (PGO)," alisema Jaji Tiganga.

Upande wa utetezi uliweka mapingamizi ya kutopokelewa kwa kielelezo cha sare za JWTZ, JKT na ramani za vituo vya mafuta, zinazodaiwa kukutwa kwa mshtakiwa wa kwanza Halfani Bwire.

Upande huo pamoja na mambo mengine ulidai shahidi wa nane, SP Jumanne Malangahe, hakueleza mnyororo wa jinsi vielelezo hivyo vilivyokamatwa, kutunzwa hadi kufika mahakamani, alama zilizowekwa sio sahihi na hakuna risiti ya kuonyesha mali zilizokamatwa.

Akitoa uamuzi huo, alisema hoja kuhusu mnyororo wa kuwasilisha kielelezo ilitolewa na Wakili Peter Kibatala na jopo lake lote na hoja ni namna kielelezo kilivyokamatwa, kutunzwa na kufika mahakamani.

Alisema kifungu cha 246 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na kanuni ya nane ya mwaka 2016, inaeleza kwamba vielelezo vyote vilivyosomwa katika maelezo ya mashahidi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ni ambavyo Mkurugenzi wa Mashtaka nchini atataka kuvitumia.

"Hakuna sheria inayosema kila kielelezo kinatakiwa kiletwe mahakamani ni wazi atakuwa amepitia kielelezo cha notebook nyekundu na kuona kama kinatengeneza kesi au hakitengenezi kesi.

"Sio lazima kwa ushahidi au shahidi aliyeorodheshwa na kutajwa katika maelezo ya mashahidi aje kutoa ushahidi mahakamani, kwa mazingira hayo mahakama inaona pingamizi kwamba notebook iliyosemwa katika maelezo ya mashahidi sio iliyoletwa mahakamani, haina mashiko inatupiliwa mbali," alisema Jaji Tiganga.

Jaji Tiganga alisema hoja ya mnyororo wa kielelezo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine mahakama ni lazima itazame sana.

Alisema endapo mnyororo huo unavunjika, basi upande wa mashtaka wanakuwa wameshindwa.

"Shahidi aliyekuja kutoa ushahidi alieleza alivyokamata mali, lakini hakubaki navyo alikabidhi kwa Sajenti Johnson, kwa kuwa bado upande wa Jamhuri hawajashindwa kumuita Sajent Johnson kutoa ushahidi, hatuwezi kusema shahidi aliyekuwapo mahakamani ameshindwa kuonyesha mnyororo wa ushahidi.

"Kuhusiana na mwaliko niliopata kutumia kesi ya Mkoka na Mayala Mbiti, nakubaliana na upande wa utetezi kuwa kanuni zilizotumika katika mashauri hayo ni mazuri lakini ikumbukwe yalifanyika baada ya ushahidi kutolewa," alisema.

Alisema mahakama inaona hoja za utetezi zimeletwa kabla ya wakati labda kama zingeletwa wakati wa majumuisho ya mwisho na kwa sababu hiyo mahakama haiwezi kuzingatia na kutupilia mbali pingamizi hilo.

"Ikumbukwe shahidi aliyekuwapo mahakamani ndiye alifanya upekuzi, hoja ya Wakili John Mallya aliomba mahakama notebook ambayo ilisomwa katika maelezo ya ushahidi Mahakama ya Kisutu sio kilicholetwa mahakamani, Mahakama inaona ilikuwapo na iliorodheshwa na karatasi zimo ambazo zina michoro, mahakama inaona hoja hiyo sio ya msingi," alisema.

Alisema vielelezo vinavyotakiwa kutolewa mahakamani viliwekwa katika furushi na kuwekwa alama ya X kumwezesha shahidi kuvitambua.

"Mahakama inaona hoja zote zilizoletwa na upande wa utetezi hazina mashiko isipokuwa hoja mbili, ya alama katika kielelezo na risiti inayotolewa baada ya kukamata mali.

"Mahakama inaona kutotolewa kwa risiti kuna athari, kushindwa kutoa risiti ni kosa na jambo hili lina athari, panapokuwa pamefanyika upekuzi kwenye nyumba, box au eneo, ofisa ambaye kakamata mali anatakiwa kutoa risiti kuhusu mali alizokamata, hati ya kukamata mali haiwezi kuwa mbadala wa risiti," alisema.

Alisema PGO inaelekeza kwamba, vielelezo ambavyo ni nguo vinatakiwa kuwekwa alama kwa kamba ambayo itapita katika vishikizo na ining'inie na eneo la kuweka alama limeelekezwa.

"Kielelezo ambacho kinatakiwa kuwekwa alama kinatakiwa kubanwa na pini, alama hiyo inatakiwa kuwa na namba, kutokana na maelezo hayo kisheria, yaliyoelezwa katika PGO hiyo ni wazi kuwa alama iliyowekwa sio alama ambayo PGO 229 imeitambua na kuelekeza," alisema Jaji Tiganga.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Bwire, Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi za kulipua vituo vya mafuta, kukata miti barabarani ili kuonyesha nchi haitawaliki.

## TEF yamtwisha 'mzigo' Nape

**Na Elizabeth Zaya**

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF) limesema limepokea kwa matumaini uteuzi wa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, huku likimtwisha jukumu la kuanza nalo la kufungua vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa.

Pia, jukwaa hilo limempongeza kwa kuteuliwa katika wizara nyingine, aliyekuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji.

Kadhalika, limempongeza aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu, Dk. Jim Yonaz kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

"Tumefanya naye kazi vizuri na kwa ukaribu katika mchakato wa kurekebisha Sheria za Habari, ambaye sasa tunaamini mchakato huu unaendelea kuwa katika mikono salama," alisema Mwenyekiti wa TEF," Deodatus Balile.

Pia limempongeza Mohamed Hamis kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari huku likimpongeza Dk. Zainab Chaula, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ambaye sasa ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Mahitaji Maalum.

"Hakika Dk. Chaula alifanya kazi kubwa ya kupigiwa mfano hasa katika mchakato wa marekebisho ya Sheria za Habari na kuyarejeshea leseni magazeti yaliyofungiwa," alisema Balile.

"Hadi sasa utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya Juni 28, 2021 kuwa vyombo vya habari vilivyofungiwa vifunguliwe unaendelea kwa magazeti ya Mwanahalisi, Mawio, Mseto na Tanzania Daima.'

Jukwaa hilo lilimpongeza Rais Samia kwa kuunda Baraza la Mawaziri, na kwamba linaamini mawaziri walioteuliwa katika kila wizara watakuza uhuru wa kupata habari, uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kutoa mawazo, ambazo ni haki za msingi zinazowezesha haki nyingine kupatikana kwa mwanadamu ambalo ni nguzo ya maendeleo ya kweli kwa kila nchi. TEF lilisema linaamini kwamba Nape atasaidia katika mchakato huo uliokwishakuanza wa kufungulia magazeti yaliyokuwa yamefungiwa.

"Tunamkaribisha Nape katika wizara hii na tunaamini atatusaidia kusukuma kwa kasi mchakato wa kuyafungulia magazeti tuliyoyataja, huku akiupa msukumo mpya mchakato wa kubadili sheria zinazosimamia taaluma ya habari kwa nia ya kukuza uhuru na kukuza uhuru wa vyombo vya habari nchini.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# SALAMU ZA PONGEZI

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), tunawapongeza Viongozi wetu wote wa **Wizara ya Fedha na Mipango** mlioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Samia Suluhu Hassan.**



**Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb),**
Waziri wa Fedha na Mipango



**Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb),**
Naibu Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango



**Bw. Emmanuel M. Tutuba**
Katibu Mkuu
Wizara ya Fedha na Mipango



**Bi. Amina Khamis Shaaban**
Naibu Katibu Mkuu-Madeni,
Wizara ya Fedha na Mipango



**Bw. Lawrence N. Mafuru**
Naibu Katibu Mkuu-Sera,
Wizara ya Fedha na Mipango

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tujifunze kuhifadhi chakula wakati wa shida

**BEI** ya mahindi katika masoko mbalimbali mikoa ya Kanda ya Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara) imepanda kutoka Sh. 55,000 hadi 127,000 gunia la kilo 100.

Pia zao hilo linadaiwa kuadimika katika baadhi ya maeneo na kuomba chakula cha msaada hasa kwa wananchi wa maeneo ya Longido.

Bei zilianza kupanda tangu mwezi Desemba mwaka jana, na sababu kubwa ikielezwa kutokana na kupungua kwa mvua, jambo lililosababisha mavuno kuwa hafifu tofauti na matarajio.

Kupanda kwa nafaka hiyo kumesababisha unga kupanda kutoka Sh. 1,000 kwa kilo moja hadi 1,200 hali inayopandisha hali ya maisha kwa wengi ambao hutegemea kama chakula kikuu.

Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa mvua ilikuwa chache na kuchelewa kiasi cha mahindi na mazao mengine kukauka kabla ya wakati, au kushindwa kustawi kiasi cha kutotoa mazao.

Hali hiyo imeathiri nchi nyingi duniani kiasi cha Kenya kutangaza ukame kama janga la kitaifa kwa kuwa binadamu, wanyama na viumbe wengine wamekufa kutokana na kukosa maji na chakula.

Chakula husafirishwa kwenda Kenya, lakini hupelekwa pia Somalia na Ethiopia ambazo sehemu kubwa ya nchi inakabiliwa na ukame na kutegemea chakula kutoka nchini.

Hakuna ubishi kuwa maeneo mengi ya Tanzania yana ardhi yenye rutuba ifaayo kwa kilimo na hulisha nchi nyingi ikiwamo Kenya na ndiyo maana vyakula vingi husafirishwa kwenda huko.

Hali ya ukame imekuwa tishio maeneo mengi kwa sasa, pia mvua hazitabiriki kiasi cha wakulima kushindwa kujua ni wakati gani walime na aina ya mazao, hapa ndipo unakuja umuhimu wa kusisitiza kilimo cha mazao yanayostahimili ukame ambayo yatafaa kwa chakula.

Wafanyabiashara hunusa harufu ya faida kwa haraka na kwa kuwa tupo kwenye soko huria basi wanaruhusiwa kuuza na kununua wanapotaka ikiwamo nje ya nchi na ndicho kilichofanyika.

Wapo wanaouza mahindi mabichi ambayo huchemshwa au kuchomwa, na wengine husubiri na kuuza mahindi makavu ambayo hutumiwa kwenye ugali, uji na vyakula vingine muhimu kwa binadamu na wanyama.

Kwa sasa mahindi kuadimika maana yake yamefichwa kusubiri bei kupanda au yamesafirishwa kwa wingi kwenda nje ya nchi, na sasa inatakiwa kuchukua hatua madhubuti.


Tunaamini akiba ya chakula iliyopo Ghala la Taifa la Chakula (NRFA), itatumika kusaidia wananchi wenye uhitaji kwa sasa kununua kwa bei nafuu, ikiwa ni pamoja na Waziri wa Kilimo kufuatilia kwa karibu ikiwa ni pamoja na kitengo cha maafa kuanza kutambua wenye uhitaji na kupeleka msaada.

Ni muhimu kuelimisha wakulima kuwa wasiuze mazao mabichi bali waone umuhimu wa kuuza baada ya kukomaa, lakini kuhimiza kilimo cha umwagiliaji kwa kuhifadhi maji ya mvua ili kukabili hali ngumu wakati wa ukame.

Pia ni muhimu kuangalia uwezekano wa kutosheleza soko la ndani kabla ya kuruhusu mazao hayo kusafirishwa nje, kwa kuwa tangu mipaka ifunguliwe watu wameendelea kusafirisha nje na kusahau kuacha akiba ndani.

Aidha, tunajua ni wakati wa soko huria lakini bado tuna wajibu wa kuhakikisha hatuuzi chakula chote na kukosa akiba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Ani-Jozeni

# Rais Samia alivyodhihirisha yuko madarakani, habahatishi

**KUJIUZULU** Spika wa Bunge, Job Ndugai ambaye ni mbunge mkongwe wa Kongwa, ni kielelezo thabiti cha kiwango ambacho Rais Samia Suluhu Hassan, amefaulu kushika hatamu za uongozi, kupitia utii wa taasisi za nchi na jumuiya za chama tawala.

Imedhihirika kuwa hategemei huruma za kuwa na haki ya kikatiba ya kutawala, au kupanga anachofanya kulingana na hisia za makundi tofauti katika CCM, jambo ambalo lilikuwa wazi wakati wa awamu ya nne ya Rais Jakaya Kikwete. Kwa njia hiyo Rais Samia amefaulu kuchukua uongozi na kuudhibiti kama mtangulizi wake, hayati John Magufuli, ambaye hakutumia uhuru wa siasa za makundi kwenye chama.

Kwa upande mwingine, kujiuzulu kwa Spika Ndugai kumewapa 'mfupa' mwingine wapinzani wa kutafuta katiba mpya, kwani kosa la Spika ni kutofautiana na Rais Samia kuhusu madeni ya nje na athari za hali hiyo. Wanaharakati wa katiba mpya wanaona tukio hilo kama kielelezo cha kutokuwapo kwa uhuru wa kujieleza katika bunge na hivyo kuwepo hitaji la hali hiyo kutolewa ufafanuzi na mwelekeo tofauti kikatiba.

Ni suala ambalo litaendelea kuwagawa wanaharakati hao na walio wengi ambao wanatambua umuhimu wa nidhamu katika uongozi wa juu, ambako Ndugai hawezi kuhitilafiana na Rais halafu abakie kuongoza.

Yako maeneo kadhaa ya siasa za Tanzania kwa wakati huu ambayo yamefafanuliwa na tukio hilo, muhimu zaidi likiwa hili la kutambua uwepo kikamilifu wa Rais Samia katika uongozi, hivyo wenye mipango mingine kwa ajili ya uchaguzi mkuu 2025 wakijikuta wana kibarua kigumu. Hatua kwa hatua nchi nzima, na zaidi kwa upande wa makundi ya vijana wa CCM, yanaapa kwa jina la Rais Samia, wakati washindani wake katika CCM bado wamejikita katika urais wa JPM, wakipima kama Samia 'anatosha' kwa viatu hivyo, lakini mwangwi huo sasa utafifia.

Tukio la kujiuzulu kwa kutokukubalika katika chama baada ya kumkosoa, na akakiri mwenyewe kuwa alipotoka katika kauli zake, ni utambulisho wa uthabiti wa uongozi katika CCM, na dhamira ya kubakiza hali hiyo siku zote.

Ndiyo maana ya 'kazi iendelee,' siyo tu kuwa miradi ya maendeleo iendelee kufuatiliwa ila itikadi ya kazi, utii na uhakika wa kufuata taswira iliyowekwa na kiongozi mkuu inabaki pale pale, kwani ikivurugwa kazi haiwezi kuendelea. Ni jibu kwa wale waliokuwa wanatazamia upenyo wa uhuru kisiasa tofauti na awamu ya tano uonekane ndani ya CCM pia, wakati ambapo vihatarishi vya uthabiti wa dola ndani ya uhuru mpana havitoki upinzani ila CCM, hasa serikalini na mashirika ya umma, wakiutumia upinzani.

Unaweza kusema kuwa kujiuzulu kwa Spika Ndugai ni kielelezo kuwa licha ya juhudi za kupata mwafaka wa jinsi ya kufanya siasa za wazi kistaarabu, si ajabu hali iliyopo ikaendelea hadi 2025 wakati wa kujiandaa kwa uchaguzi mkuu. Tukio hili limezua changamoto nyingine katika mkakati wa kupanua wigo la uhuru wa kisiasa kwani kimsingi inaonekana kuwa CCM pia wana jambo lao, badala ya kubakia muafaka kati ya CCM na upinzani. Hivyo kuzuia upinzani kufanya harakati za wazi ni athari tu za lengo kubwa zaidi, yaani kuzuia viashiria vya mpasuko katika chama tawala, hali inayoweza kumsumbua Rais Samia kwa kina zaidi kuliko kauli za wapinzani.

Ukiangalia kwa karibu unakuta kuwa hatima ya Ndugai ilipigwa muhuri na watu wa makundi mawili yenye mielekeo tofauti, kwanza kundi la viongozi wa UVCCM ambao ni watiifu kwa Rais Samia, wakikosa imani na Spika baada ya alichosema, alivyotubu na kukosolewa kwa dhati, tena hadharani na Rais.

Kundi lingine ni la wafuasi wa Ndugai, vinara wa makundi ya bunge ambao walimwona ni shujaa kwa yale aliyosema, kama alivyokiri Askofu Josephat Gwajima, kuwa alipotoa kauli zake kuhusu deni la taifa, alimpelekea ujumbe akisema ndiye Ndugai ninayemfahamu. Alipoomba radhi aliwaacha watani zake, Wasukuma akidai yeye hayumo humo - na ni wazi alimtaka aachie ngazi kwa sababu siyo shujaa tena.

HABARI KITAIFA






Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, akizungumza baada ya kukabidhiwa vyumba vya madarasa mapya ya sekondari 94 na shule shikizi 28 na Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mjini, Mohamed Moyo (wapili kulia), katika hafla iliyofanyika hivi karibuni, Sh. bilioni 3.3 za UVIKO-19 zilitumika katika ujenzi huo. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Kabanga, BHP kuwekeza Dola milioni hamsini

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kabanga Nickel Limited ya nchini Uingereza, kwa kushirikiana na kampuni ya BHP imewekeza zaidi ya Dola za Marekani milioni 40, kwa ajili ya kuharakisha ujenzi wa mradi wa nikeli salfaidi nchini.

Aidha, kampuni ya BHP imewekeza Dola milioni 10 kwenye kampuni ya Lifezone Limited ili kukuza usambazaji wa teknolojia yake yenye hatimiliki katika uchenjuaji wa madini iitwayo "hydrometallurgy" (hydromet).

"Teknolojia ya hydromet kutoka Lifezone ni ya gharama

nafuu zaidi kuliko uchenjuaji kwa kuyeyusha, ina athari ndogo zaidi katika mazingira, na

itahakikisha kuwa madini ya nikeli yanayotumika kutengeneza betri, madini ya shaba na kobalti

yanazalishwa nchini Tanzania," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Kabanga Nickel, Chris Showalter.

"Tuna furaha kutangaza ushirikiano huu unaonyesha jinsi madini yaliyopo Kabanga yalivyo na hadhi kimataifa na umuhimu wake katika kusaidia kukabiliana na changamoto ya hewa ya ukaa inayokabili dunia hivi sasa."

Alisema BHP ni mshirika sahihi kwa Kabanga Nickel, kwa kuwa ina mbinu na utaalamu mkubwa utakaowezesha mradi kusonga mbele hasa katika kulinda mazingira katika mnyororo wa thamani wa nikeli.

Kwa mujibu wa Showalter, ufadhili wa BHP katika teknolojia ya uchenjuaji ya 'hydromet' kutoka Lifezone, ni suluhisho la uchenjuaji endelevu wa madini, utasukuma harakati za uhifadhi wa mazingira.

Alisema kupitia ujenzi wa Kabanga na teknolojia ya hydromet kutoka Lifezone, Tanzania itakuza nafasi

yake katika uzalishaji wa madini yanayotumika kutengeneza betri ambayo ni muhimu katika kufikia

uchumi wa dunia wenye kiwango cha chini cha hewa ya ukaa."

Alisema uwekezaji katika kampuni ya Kabanga Nickel

BHP itawekeza dola za Kimarekani milioni 90, katika hati fungani zinazoweza kubadilishwa ndani ya Kabanga Nickel katika awamu mbili:

Alisema ni uwekezaji wa awali wa Dola za Kimarekani milioni 40, ukifuatiwa na uwekezaji mwingine wa dola

milioni 50 baada ya makubaliano kufanyika na kutimizwa kwa masharti mengine.

Showalter alisema baada ya kukamilisha taratibu zote za kisheria nchini, awamu ya kwanza ya Dola za

Marekani milioni 40 itabadilishwa na kuwa asilimia 8.9 ya hisa za Kabanga Nickel (Asilimia 7.5 ya

faida za Tembo Nickel Corporation ("Tembo"). Baada ya kuwekezwa na kubadilishwa kuwa hisa,

fedha za awamu ya pili Dola za Kimarekani milioni 50 zitaongeza hisa za BHP katika KNL kufikia

asilimia 17.8 (Asilimia 15.0 ya faida za Tembo), na kufanya thamani ya mradi huo kufikia dola

za Kimarekani milioni 658.

Alisema baada ya kukamilika kwa masharti mengine, BHP itapata haki ya kufanya uwekezaji zaidi katika

Kabanga Nickel baada ya kufikia hatua zilizokubaliwa, na kwamba uwekezaji huo hautahamisha haki za uendeshaji na usimamizi wa mradi kutoka kwa Kabanga

Nickel Corporation kupitia kampuni ya ubia hapa nchini ya Tembo Nickel Corporation.

Aidha, ujenzi wa mradi unatarajia kuwa uzalishaji utaanza kufanyika mwaka 2025, na kwamba uzalishaji utaongezeka kufikia tani 40,000 za nikeli na tani 6,000 za shaba pamoja na tani 3,000 za kobalti kwa mwaka.

Katika hotuba yake kwenye mkutano wa COP26 mjini,

Glasgow, Scotland, Novemba mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan alisisitiza haja ya nchi zilizoendelea

kulisaidia bara la Afrika katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, alisema;

"Tanzania ina ndoto ya kuwa kitovu cha madini yanayowezesha kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa. Ninafurahi kwamba Kabanga Nickel inatambua fursa hii na inawekeza katika mustakabali wetu." alisema.

Alisema kupitia kazi ya Kabanga Nickel, na rasilimali za nchi kuna utayari wa kuweka mchango duniani katika uzalishaji na usafirishaji wa metali muhimu zinazohitajika katika jamii huku kukiwa na ajira na kukuza uchumi.

thps
Tanzania Health Promotion Support

## PUBLIC AUCTION FOR USED VEHICLES

**PUBLIC AUCTION FOR USED VEHICLES**

Tanzania Health Promotion Support (THPS) is an indigenous NGO established under non-governmental organization act No 24 of 2002 in 2011. THPS works in partnership with the Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children (MOHCDGEC) and Regional Administration and Local Government (PORALG), The Ministry of Home Affairs and Ministry of Health (MoH) in Zanzibar with a goal of ensuring accessible high-quality health care services to Tanzanians; through strengthening of health and community systems for comprehensive quality health services including HIV/AIDS; Tuberculosis; prevention of GBV; reproductive, maternal, neonatal, child, and adolescent health (RMNHCAH) services; laboratory and health management information systems (HIMS).

Tanzania Health Promotion Support (THPS), located at Coco Plaza building 3rd floor, through MAJEMBE AUCTION MART intends to offer for sale its used vehicles at Public Auction to the highest bidder the below listed used vehicles. The auction will be on Saturday 22nd January 2022 at Masaki area, in the open space near Coco Plaza building as from 10:30AM.

**The used vehicles are as shown on the list below.**

| S/N | Tender Reference No. | TYPE OF USED VEHICLE | REG.NO | STATUS |
|---|---|---|---|---|
| 1. | THPS/VDSP/2021/01 | Toyota RAV4 S/Wagon | DFP 8365 | Running |
| 2. | THPS/VDSP/2021/01 | Nissan Patrol S/Wagon | DFP 5604 | Grounded |
| 3. | THPS/VDSP/2021/01 | Nissan Patrol S/Wagon | DFP 5808 | Running |

**AUCTION REQUIREMENT**

1. The vehicles are sold on "as is" basis and Tanzania Health Promotion Support, (THPS) shall have no further liability after sale.
2. Vehicles may be inspected from 08:00 to 16:30Hrs as from Wednesday 19th January, 2022 to Friday 21st January 2022.
3. The buyer shall pay 25% of the agreed price either on the auction day or on the deadline of 24th January 2022 at 1:00Pm, while the remained amount shall be paid within 14 days from the auction day otherwise the process will be repeated and the 25% of the total amount paid will not be refunded. Payment shall be deposited to Tanzania Health Promotion Support (THPS) Account Number: 0150237214202, CRDB Bank, Oysterbay Branch and only payment slip will be submitted as a proof of payment. No cash transaction will be allowed,
4. The buyer will be allowed to take the vehicle(s) after paying the full amount of the agreed price and buyer shall be fully responsible for paying ALL taxes (including VAT) and any other charges which may arise from the purchase of the vehicle (s). The buyer will present the plate numbers and all documentations as evidence that he/she has paid all the required taxes during taking the vehicle at THPS premises.

**For more information, please contact:**
**THE CHIEF OPERATIONS OFFICER**
**TANZANIA HEALTH PROMOTION SUPPORT**
**COCOPLAZA BUILDING, 3RD FLOOR**
**P.O.BOX 32605**
**DAR ES SALAAM**

**TELEPHONE: NO. +255-22-2923107**
**FAX +255-22-2923108**




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati) pamoja na viongozi wengine akiwamo Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (wapili kulia), wakati Wimbo wa Taifa ukipigwa kabla ya uzinduzi wa Kikosi Kazi kitakachopitia hoja zilizojitokeza katika mkutano wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, jana Zanzibar. PICHA: IKULU

# Rais Mwinyi apongeza kukomaa kwa demokrasia

**Na Waandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema viongozi wa vyama vya siasa kukaa pamoja ni kielelezo cha kukomaa kwa demokrasia nchini.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua kikosi kazi kitakachopitia hoja zilizojitokeza katika mkutano wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa Tanzania uzinduzi ambao umefanyika, mjini hapo.

Alisema utamaduni wa Watanzania wa viongozi wa vyama vya siasa kukaa pamoja kujadili masuala muhimu ya uchumi wa nchi ni kielelezo imara cha kukomaa kwa demokrasia na uimara wa kuendeleza Serikali ya Umoja wa Kitaifa na mshikamano wa wananchi.

Alisema kwa pamoja nchi imepata mafanikio katika kipindi cha miaka 29 tangu nchi iliporuhusu mfumo wa vyama vingi, pia zipo changamoto kadhaa ambazo zimejitokeza zinazopaswa kufanyiwa kazi.

Alisema kikosi kazi hicho kilichowashirikisha wataalamu wabobezi katika masuala ya uongozi, usuluhishi wa migogoro, haki za binadamu, utawala bora na masuala mbalimbali, inampa matumaini kwamba maamuzi yatakayopitishwa yataleta maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii nchini.

Alisema Serikali ya Zanzibar na Tanzania zitatoa ushirikiano kwa kikosi kazi hicho ili kukamilisha majukumu waliyopewa.

Alisema maendeleo ya nchi yanahitaji amani na utulivu uliopo na kuendelea kwa amani hiyo kunahitajika maridhiano ya kweli baina ya vyama vya kisiasa.

Alisema masuala ya kisiasa yanagusa hisia za wananchi na wananchi wanapikwa na kufahamu matamko na kauli za wanasiasa kwa upeo na muono tofauti.

Aliwataka wanasiasa kila wakati kuwa makini na kauli wanazozitoa na kuhakikisha sera za vyama vya siasa zinazingatia na kuhakikisha kuwaunganisha Watanzania na sio kuwagawa.

Aliwataka viongozi hao kutumia hekima na busara, uzalendo na uzoefu wao katika uchambuzi watakaofanya na kuwa tayari kubatilisha hoja ambazo wanahisi kuleta mgongano au kuwa kikwazo kwa maendeleo ya nchi.

Aliwataka kuweka pembeni tofauti zao na kufanyakazi kwa kuzingatia maadili na kanuni zinazoongoza kikosi hicho ili kuzingatia maslahi ya taifa.

Dk. Mwinyi alisema siasa ni uwanja mpana uliojengwa kwa tafsiri mbalimbali na kuwasihi kuzitumia tafsiri hizo kwa wanavyozifahamu kwa kuzingatia maslahi ya Tanzania.

Alisema historia ya Tanzania ni ya kipekee na yakupigiwa mfano duniani kote kutokana na muungano, umoja na mshikamano, wanavyochambua hoja zinazozingatia kuendeleza Muungano na Mapinduzi ya Zanzibar na kuimarisha misingi ya umoja na mshikamano.

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, kwa upande wake alisema kikosi hicho kinafanya kazi kubwa ya kujenga mustakabali mpana wa nchi.

Alisema kila Mtanzania anayethamini maendeleo ya nchi kikosi hicho ni uwekezaji mkubwa kwa manufaa ya nchi na kila mmoja athamini hatua hiyo.

Vile vile, alisema kikosi hicho kimejumuisha makundi mbalimbali ikiwamo vyama vya siasa na kukumbuka kwamba kuna Watanzania waliokuwapo Tanzania na nje hivyo kuchukua juhudi ya kuwashirikisha ili kuleta tija kwa kikosi hicho na kupatikana kile kilichokusudiwa.

Mapema Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, alisema katika kutekeleza majukumu yake, kikosi hicho kimepewa kazi mbalimbali ikiwamo kupitia hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Mwinyi, wakati wakihitimisha masuala ya wadau.

Kazi nyingine ni kupitia na kuchambua maoni yote yaliyotolewa katika kikao cha wadau wa vyama vingi uliofanyika Desemba 15 hadi 17, mwaka jana na kuandaa mapendekezo kuwasilisha serikalini ambayo yatahitaji kutekelezwa mara moja.

Eneo lingine alisema ni kupendekeza mambo bora ya kuandaa utaratibu mzuri wa kuzungumza mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kwa lengo la kupata suluhisho kwa chagamoto zinazojitokeza.

Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Reseach and Education for Democracy in Tanzania (REDET), Profesa Rwekaza Mukandara, aliwapongeza viongozi wa nchi kwa utayari wao wa kutafuta suluhisho la changamoto za kisiasa na kijamii zinazolikabili taifa kwa mazungumzo, mashauriano na makubaliano.

Alisema kazi iliyo mbele yao ni muhimu na ngumu na waliahidi kufanya kazi kama walivyoelekezwa kwa kuwa jukumu hilo lina mambo nyeti katika nchi ikiwamo Katiba mpya, Tume Huru ya Uchaguzi, vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara na kuendesha shughuli zao kwa uhuru na mambo mengine.

Waliahidi kutumia mchakato jumuishi ili mapendekezo yote yaweze kukidhi kiu ya kuwa na nchi yenye amani, utulivu, haki, siasa za kistaarabu, utawala bora na maendeleo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili, Sera, Uratibu na Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohammed, aliwapongeza wajumbe wa kamati na kwamba hana mashaka na kikosi hicho kwa kuwa ni wajumbe makini, wenye weledi na kitafanya kazi vizuri kwa kuzingatia maslahi mapana ya taifa.

Aliahidi Ofisi ya Waziri Mkuu ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Makamu wa Pili itahakikisha itatoa kila aina ya ushirikiano kwa kamati hiyo ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.

**KIKOSI KAZI**

Aidha, Chama cha ACT-Wazalendo, kimezindua kikosi kazi cha kuchambua hoja zilizoibuliwa kwenye mkutano wa wadau wa siasa, uliofanyika jijini Dodoma, Desemba mwaka jana.

Kaimu Mwenyekiti wa chama hicho, Dorothy Semu, katika taarifa yake jana, alisema mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa kikao hicho, alikuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, huku Zitto Kabwe, kiongozi wa chama, akiongoza ujumbe wa chama.

Alisema, waliohudhuria wengine ni Salim Bimani, Katibu Mwenezi Taifa na Ndugu Pavu Abdallah, Naibu Katibu wa Haki za Binadamu.

"Sisi ACT-Wazalendo tutashiriki katika Kikosi Kazi kupitia Kiongozi wa chama, Zitto Kabwe, ambaye ameteuliwa kuwa mjumbe. Masuala muhimu tutaendelea kuyasimamia na kuyasisitiza; kuandikwa kwa sheria mpya ya uchaguzi, itakayoifanya Tume ya Uchaguzi kuwa huru, yenye weledi na inayoaminika," alisema Semu.

"Kuandikwa kwa sheria mpya ya kuwezesha vyama vya siasa kufanya kazi zake kwa uhuru bila bugudha na kuimarisha mfumo wa demokrasia ya vyama vingi nchini; kuandaa kalenda inayoeleweka na kutekelezeka kukamilisha mchakato wa Katiba Mpya.

Pia alisema chama kitashiriki kurekebishwa kwa sheria kandamizi zinazominya uhuru wa wananchi na kuwekwa kwa utaratibu wa kuwa na mchakato wa maridhiano ya kitaifa kwa kuhusisha wadau wote ikiwamo kutazama njia bora za kuhakikisha ushirikishwaji wa wadau wakuu katika serikali ili kujenga umoja wa kitaifa.

**Imeandikwa na Christina Mwakangale DAR, Rahma Suleiman, Zanzibar**

HABARI KITAIFA

## CEGODETA yampongeza Ndugai kujiuzulu

**Na Sabato Kasika**

TAASISI ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), imempongeza aliyekuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Job Ndugai kujiuzulu nafasi hiyo, kitendo walichokiita ni cha kiungwana.

Imesema ni vyema viongozi wa umma wakazingatia utaratibu wa kuachia ngazi pale 'wanapojikwaa' badala ya kusubiri kushinikizwa na umma.

Akitoa salama za mwaka mpya za taasisi hiyo jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti Thomas Ngawaiya alisema, wadhifa aliokuwa nao Ndugai, suala la kujiuzulu halikuwa na mjadala.

"Hata kama Rais angemsamehe, alikuwa tayari ameshachafua hali ya hewa, njia pekee ya kulinda heshima yake ilikuwa ni kujiuzulu, hivyo nasi CEGODETA tunampongeza kwa uamuzi huo," alisema Ngawaiya.

Alisema, kujiuzulu kwa Ndugai kuwe ni fundisho kwa viongozi wengine ambao wamekuwa wakikumbwa na tuhuma mbalimbali na kuendelea kung'ang'ania madaraka.

"Umefika wakati pia viongozi kutosubiri mashinikizo ndipo waachie ngazi, wanapogundua kuwa wamefanya makosa, njia nzuri ni kuachia ngazi mara moja," alisema.

Aidha, katika salamu za mwaka mpya za taasisi hiyo, Ngawaiya alitoa wito kwa serikali kuboresha demokrasia ya vyama vingi na pia kuwapo kwa mchakato wa Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi.

Alisema, serikali imeongeza wawekezaji kutoka nje kwenye sekta ya viwanda, kuinua uchumi kuongeza ajira na kuboresha uhusiano na biashara kati ya Tanzania na nchi jirani na kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Jumuiya za Kimataifa.

"Sisi kama wadau wa utawala bora, tunatoa wito kwa serikali kuendelea kuboresha demokrasia ya vyama vingi na pia kuwapo kwa mchakato wa Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi," alisema.

Vile vile, alisema kuwa taasisi yake inawataka Watanzania kuhamasisha mazuri yote yaliyofanywa na serikali za awamu zilizopita na iliyopo sasa, kwa manufaa ya kizazi kilichoko na kijacho.

# Kemikali iliyomwagika na kuleta madhara yaondolewa

**Na Idda Mushi,** MIKUMI

OFISI ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), wameondoa takribani tani tatu za kemikali aina ya Sulphur iliyokuwa imemwagwa katika barabara kuu ya Morogoro-Iringa, eneo la kijiji cha Msimba, Mikumi Januari 6, mwaka huu.

Kemikali hiyo ilimwagika wakati lori lililokuwa safarini kupata ajali na kusababisha wananchi kuugua magonjwa mbalimbali ikiwamo macho, kifua na ngozi.

Waandishi wa habari waliotembelea eneo hilo, walishuhudia kemikali hiyo ikiwa imehifadhiwa kwenye mifuko ya sandarusi maarufu kama kiroba, ndani ya gari aina ya fuso, tayari kupelekwa kuteketezwa jijini Dar es Salaam.

Meneja kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya Kati, Mussa Kuzumla, alisema wanaosimamia utekelezaji wa sheria ya usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani, kuanzia inapoingizwa, kusafirishwa na kwenda kutumika, walipata taarifa kutoka NEMC kuhusu ajali ya lori lililokuwa likisafirisha kemikali, tangu Januari 6, mwaka huu.

"Hadi sasa kwa makadirio tumeweza kuondoa kiasi cha tani tatu cha kemikali hii katika eneo hili na msafirishaji ambaye sisi ndiye ambaye tunamtambua, tumeshamfungulia jadala kutokana na makosa aliyofanya na taratibu za kumfikisha mahakamani zinaendelea," alisema.

Alitaja makosa anayotuhumiwa nayo ni pamoja na kutotoa taarifa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkemia Mkuu wa Serikali ili wasimamie uondoaji wa kemikali hiyo katika eneo la ajali, kutumia wananchi wasio na elimu kuizoa na kosa la tatu ni kuzoa kemikali anayoihitaji na kuacha nyingine katika eneo la ajali na kuondoka.

Alitoa wito kwa wananchi kutoa taarifa kwa Ofisi ya Mkemia Mkuu na vyombo vingine vya ulinzi na usalama wanapobaini kemikali katika maeneo yao.

Kuhusu athari kwa wananchi kutokana na kemikali hiyo ya Sulphur, alisema madhara ya papo kwa papo yamekuwa ni kwenye ngozi na macho, ya muda mrefu kwa wanaofanya kazi kwenye mazingira ya kila siku na ya muda mrefu ni kuathirika kwa mfumo wa fahamu na magonjwa ya kifua kama pumu.

Mwakilishi wa NEMC kutoka kanda ya Morogoro Rufiji, Jane Kadoda, alisema kwa kufuata kanuni za mazingira na sheria zake, eneo hilo liliwahusu ndiyo maana wakamtafuta aliyetoa kibali cha kusafirisha ambaye ni Ofisi ya Mkemia Mkuu ambao wanaujuzi wa kilichokuwamo katika mzigo huo na msafirishaji wake, wakatafuta vifaa vya kuiondoa hadi kuweka eneo hilo katika mazingira salama ya awali.

"Na kwa vile kemikali hii ina tabia ya kutoyeyuka kwenye maji kwa haraka, ikatusaidia, hata kama mvua ingenyesha tungeiondoa pamoja na udongo wake," alisema Kadoda.

Baadhi ya wananchi walioshuhudia akiwamo Said Mkumbila, alidai siku ya ajali, dereva aliwaomba wamsaidie kuzoa akiwaambia kemikali hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya kwenda kutengeneza soda.

"Lakini kadiri siku zilivyokwenda wanakijiji tulianza kuumwa macho, yaliwasha na kuwa mekundu, ngozi ikawa inawasha na hapa hadi tumbo nasikia linauma na kifua, lakini sisi tumezoea kusaidia watu wanaopata ajali hapa, kwa hiyo na hili tulisaidia kama tunavyosaidia watu wengine, ndiyo maana tunaomba mtusaidie kupata vipimo vya afya ili kuona kama tuko salama," alisema Mkumbila.

Kemikali hiyo ilimwagika toka Januari 6 na iliondolewa Januari 9..



Katibu Mtendaji wa Wanazuoni wa Kiislam Tanzania Ha-Atul Ulama, Shekhe Ibrahim Ghulaam (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kumpongeza Rais mstaafu, Ali Hassan Mwinyi kwa kupewa tuzo ya kimataifa ya Mfalme Feisal kwa kuhudumia uislam na waislam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Walimu waonywa kujihusisha mapenzi kazini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamewataka walimu wa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama, kuacha tabia ya kujihusisha kimapenzi na wanafunzi.

Wameshauri mwalimu atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo achukuliwe hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa ajira ili iwe fundisho kwa walimu wengine wenye tabia kama hizo. Imedaiwa kuwa walimu wa shule hizo wanawarubuni wanafunzi wa kike kwa kuwapatia mitihani ya somo analofundishwa na mwalimu huyo na kuwaahidi kufanya vyema kwenye mitihani na anapopata ujauzito anamkana.

Hayo yalibainishwa jana na wananchi hao wakati wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti namna wazazi walivyojipanga kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza wanaingia madarasani na wanatatua tatizo linalowakabili wanafunzi wa kike.

Omary Juma, mkazi wa kata ya Segese Halmashauri ya Msalala, alisema Jumatatu ijayo shule zitafunguliwa na wazazi wanatakiwa kutatua changamoto zinazowakabili wanafunzi wa kike. Alisema asilimia kubwa ya wanafunzi wanaopata ujauzito na kukatisha masomo yao ni waliorubuniwa na walimu wao kwa madai ya kuwapatia mitihani ya masomo wanayowafundisha na wanapopata ujauzito hukatisha masomo na wazazi kuelewana.

Naye Diwani wa Kata ya Nyamilangano, Robert Mihayo, alisema walimu kujihusisha na wanafunzi kimapenzi ni ukosefu wa maadili ya kazi, wanatakiwa kuwajibishwa kisheria na kwamba wamezoea kuona vitendo vya namna hiyo wakituhumiwa waendesha bodaboda.

Aliwataka wazazi kuacha tabia ya kuondoka asubuhi na kurudi nyakati za usiku bila ya kuangalia watoto wanaendeleaje kutokana na mimba nyingi hutokana na watu ambao wanawafahamu kwa ukaribu baina ya familia na mtu husika anayetenda tukio hilo.

Kwa upande wake, Mkaguzi wa Jeshi la Polisi na Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto, Tiho Masatu, alisema ofisi yake imekuwa ikipokea kesi mbalimbali za ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, ikiwamo wanafunzi kupata ujauzito na kukatisha masomo.

Alisema, kwa kipindi cha mwaka jana kuanzia mwezi Januari hadi Oktoba, jumla ya wanafunzi 24 kutoka shule za msingi na sekondari, walipata ujauzito wakiwa masomoni na kusababisha kushindwa kuhitimu salama na kutimiza malengo yao.

Masatu alisema katika kipindi hiki wanafunzi wengi wanapata mimba kutokana na wanaume kutojitambua na kuwa na matamanio makubwa kupita kiasi, huku akiwataka wazazi nao kutimiza wajibu wao wa kuwalea watoto katika mifumo ya maadili.

# Uamuzi mdogo kesi ya Sabaya Ijumaa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Januari 14, mwaka huu, itatoa uamuzi mdogo kama aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita wana kesi ya kujibu.

Mahakama hiyo, inatarajia kutoa uamuzi huo kama washtakiwa hao wana kesi ya kujibu au la baada ya upande wa Jamhuri kufunga kesi.

Sabaya na wenzake wanakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la matumizi mabaya ya madaraka, kuongoza genge la uhalifu na kujihusisha na vitendo vya rushwa katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayowakabili.

Mbali na Sabaya washtakiwa wengine, katika shauri hilo ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Janath Sekule, jana alidai kuwa upande wa mashtaka unaomba kufunga kesi dhidi ya washtakiwa.

"Mheshimiwa Hakimu shauri limekuja kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa, upande wa mashtaka tunaomba kufunga kesi hii dhidi ya washtakiwa," alidai Sekule.

Naye Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alidai kwamba hawana pingamizi la ombi lililoletwa na upande wa mashtaka dhidi ya washtakiwa.

Alidai kwamba baada ya kufungwa kwa kesi hiyo, Mahakama inapaswa kwa kuwaeleza washtakiwa hao kama wana kesi ya kujibu au la.

Kadhalika, alidai hawana kitu cha kujibu na wanaiomba Mahakama kupitia vielelezo vya ushahidi vilivyotolewa mahakamani na kuangalia kama washtakiwa hao watakuwa na kesi ya kujibu.

Baada ya kusikilia hoja hizo, Hakimu Patricia Kisinda, alisema kwamba Januari 14, mwaka huu, itatoa uamuzi mdogo kama watakuwa na kesi ya kujibu.

Shauri hilo la uhujumu uchumi lilisikilizwa mahakamani huko kwa takribani miezi miwili na nusu na upande wa mashtaka ukiwasilisha vielelezo vya ushahidi zaidi ya nane na mashahidi 13.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu na kujipatia Sh. milioni 90, kujihusisha na rushwa linalomkabili Sabaya na mshtakiwa wa pili, matumizi ya madaraka, utakatishaji fedha linawakabili wote.



Ujenzi wa bwawa unaendelea kwa kasi katika shamba la kibiashara la 'Farm For the Future' mjini Iringa, uwekezaji wa hekta 250 katika uzalishaji wa mahindi ya mbegu na makadamia unatarajiwa kuanza Oktoba, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka maadili ya kazi kwa watumishi

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema watumishi wanatakiwa kufanya kazi kwa kufuata maadili, kwa kuondoa urasimu sehemu za kazi ili kutokomeza rushwa.

Kunenge aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake katika Halmashauri ya Mkuranga, kuzindua mwongozo wa kupambana na rushwa utakaokuwa unatekelezwa katika mkoa huo na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa kushirikiana na skauti.

Alisema lazima ifikie wakati watumishi waone namna ya kuepuka rushwa na kufanya mambo kwa uwazi kwa kufuata maadili ya kazi na kuachana na urasimu kwenye maeneo yanayotoa huduma kwa jamii.

Alisema mkoa huo utatoa semina na mafunzo ili jamii ipambane na vitendo vya rushwa, ambavyo wakati mwingine vinakuwa kikwazo cha maendeleo.

"Mafunzo yatafanyika kwa watumishi na tutahakikisha vijana wana maadili yanayotakiwa, tutakuwa tunatenga fungu kwa ajili ya kutoa elimu kwenye maeneo ya kazi na katika jamii ya mkoa wetu," alisema.

Alisema kipato kingi kinapotea kutokana na ukosefu wa maadili na suala la rushwa kwa watumishi linaleta madhara ya kisheria yanamkuta mtu mmoja mmoja.

"Jamii yetu inatakiwa kubadilika, vijana wafundishwe maadili kwani hatuwezi kufanikiwa endapo taratibu zetu hatutazizweka vizuri katika kupambana na rushwa, na hawa TAKUKURU hawawezi kufanya kazi peke yao lazima tushirikiane," alisema Kunenge.

Kamishna Mkuu wa Skauti Tanzania, Grace Kado, alisema elimu dhidi ya rushwa itakuwa inaenezwa kuanzia shuleni kwa kushirikiana na TAKUKURU na itawafikia wanafunzi wadogo ambao watakuwa wanapatiwa elimu hiyo mara kwa mara ili wawe kuwa mabalozi kwa jamii.

Alisema kufuatia mwongozo huo rushwa, inaweza kuisha kwa kuwa klabu nyingi za kupinga rushwa zitaundwa kwa kuwashirikisha wanafunzi wadogo.

Mkuu wa dawati la elimu kwa Umma wa TAKUKURU, Fredrick Mbigili, alisema klabu za wapinga rushwa zilizopo shuleni zikishirikiana na skauti kujenga uadilifu na kuwa sehemu ya kuwaandaa viongozi waadilifu wa baadaye.

## Kampuni yakaribisha wawekezaji umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Farm For the Future Tanzania Ltd (FFF) ya mkoani Iringa, imewataka wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye ujenzi unaoendelea wa bwawa la umwagiliaji maji na miundombinu ya umwagiliaji.

Mwenyekiti na Meneja Mradi wa FFF, Osmund Ueland, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wadau wa umwagiliaji, kuwa lengo ni kuongeza kasi ya uzalishaji wa mbegu za mahindi na makadamia ambayo ni mazao yenye faida kubwa duniani.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, kampuni hiyo imekusanya Dola za Kimarekani 350,000 za kwanza kwa uwekezaji katika bwawa la ardhi, na inatarajia wawekezaji wapya watakaoongeza Dola 950,000 za ziada.

Alisema lengo ni kuweka miundombinu ya umwagiliaji na vifaa vya kuwezesha uvunaji wa maji ya mvua katika shamba la hekta 250 za mahindi ya mbegu na makadamia, unaotarajia kuanzia Oktoba 2022.

Kwa mujibu wa Ueland, umwagiliaji ni uwekezaji muhimu unaofungua fursa ya kilimo chenye tija kwa mazao yenye faida na umwagiliaji utaondoa changamoto zitokanazo na hali ya hewa.

"Kilimo cha umwagiliaji kitakuza uzalishaji wa mahindi mbegu na makadamia, ambazo ni bidhaa za thamani kubwa zenye matarajio ya kuongeza faida ya shamba na kuchangia katika kuinua kipato cha kaya katika eneo hilo kupitia mamia ya ajira shambani," alisema Ueland.

Alisisitiza kuwa uwekezaji wa mazao ya thamani kubwa utakuwa ni injini yenye nguvu katika maendeleo ya jamii zinazozunguka shamba hilo kwa kuwapa wakulima wadogo zaidi ya 2,000 na wa kati fursa ya kulima mazao hayo na litawainua maelfu ya wananchi kutoka katika umaskini.

Vilevile, shamba hilo linatarajia kutoa ajira kwa mamia ya wafanyakazi wa kudumu na wa msimu.

Ueland alisema wawekezaji katika FFF wanapaswa kufanya uamuzi wa busara kwa sababu kilimo ni uwekezaji wa muda mrefu.

"Ninaamini wawekezaji walio na dira ya muda mrefu ya uwekezaji wataona mradi huu ni wa kusisimua. Uzalishaji kamili huanza baada ya miaka saba ambapo ina maana kwamba wawekezaji watalazimika kusubiri kwa miaka mitano kwa gawiwo lao la kwanza kutoka kwenye uzalishaji wa makadamia, ingawa wawekezaji wenye malengo ya kupata faida katika muda mfupi bado watapata thamani ya juu ya kuuza mara tu baada ya upandaji kuanza Oktoba mwaka 2022."

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 11, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 12

Uhaba, ukosefu intaneti unavyotesa Afrika kimawasiliano kwenye corona



Ukurasa 14

Ni raha tupu ujenzi madarasa mapya Shinyanga kwa heri msongamano



Ukurasa 13

**Mwanasheria: Staha ya mama kazini inalindwa na sheria zake**

ELIMU

**NA DK. FELICIAN KILAHAMA**

# Inashangaza vyombo vya habari vinapoongoza kuboronga Kiswahili

• Ajabu viongozi 'Kizungu' badala ya Kiswahili...

WASOMAJI wenzangu wa Nipashe heri kwa mwaka mpya. Kumbukeni ni vyema na haki kumshukuru Mwenyezi Mungu kila wakati na hasa sasa tunapofurahia mwaka 2022 kwa amani na afya njema.

Japo 'mazoea yana taabu' lakini hili la Kiswahili cha mitaani kinatumika zaidi kuliko sanifu, ni jambo linalonigusa. Katika hali isiyotarajiwa, kuna baadhi ya maneno yanatumiwa na kutamkwa mara kwa mara kwa kujiamini kupitia baadhi ya vyombo vya habari na viongozi wa ngazi mbalimbali.

Ninaposikiliza baadhi ya vyombo vya habari, 'Kiswahili cha mitaani' kinatumika, mfano "masaa, lisaa limoja, mataa, madawa, mashule, mahospitali" yote haya yanatamkwa kama ni Kiswahili sahihi pia kuyatumia kwenye matangazo. Vilevile, kuna uzoefu wa kuchanganya Kiingereza na Kiswahili, pengine ni kwa sababu Kiswahili kinakosa baadhi ya maneno au ni ile hali ya kuonyesha umahiri wa mhusika katika kumudu English?



Utangazaji ni kazi inayoweza kuimarisha au kuharibu Kiswahili. **PICHA: MTANDAO**

Sina uhakika kama Baraza la Taifa la Kukuza na Kuendeleza Kiswahili Sanifu limeridhia maneno kama hayo yatumike. Kuna msemo wa Kiingereza: "if you can't win them join them" 'ukimaanisha 'kama huwezi kuwabadilisha au kuwashinda ungana nao' na mambo yaendelee.

Neno 'masaa' linatakiwa kuwa 'saa' hakuna haja ya kuweka 'ma' iwe ni saa moja au nyingi neno linabaki kuwa hivyo. Mathalani, sema "nimetumia saa moja au saa tatu" kumaliza kazi. Wakati mwingine utasikia mtangazaji kwenye runinga au redio, akisema tumebakiza 'lisaa limoja' kumaliza kipindi au bado 'masaa matatu' tukamilishe kipindi.

Kuna ugumu gani kwa mtangazaji kusema 'imebaki saa moja kukamilisha kipindi au zimebaki saa tatu tukamilishe kipindi'? Vilevile, huwa nasikia kwenye tangazo moja la ulinzi "masaa" 24" badala ya kusema 'ulinzi saa 24'.

Kwa upande wa taa za barabarani utasikia kwenye daladala abiria akiwasiliana na mwenzake 'tukutane kwenye "mataa" ya Ubungo'. Sijui hayo 'mataa' ni makubwa sana au ni machafu kiasi cha kusababisha yatajwe hivyo au ni ule wepesi wa kusema?

Kimsingi mhusika kutumia maneno kama hayo ni mazoea hakumbuki tena matumizi ya Kiswahili sanifu hata anapokuwa sehemu za kazi au maeneo yenye watu wengi au katika vyombo vya usafiri.

Vilevile, maneno kama "mashule" Kiswahili sanifu ni shule hata kama ni nyingi au shule zaidi ya kumi. Kadhalika, neno 'dawa' halina wingi iwe ni moja au nyingi neno ni hilo hilo, imekuwa kawaida kuona duka linalouza dawa limeandika "duka la madawa" wengine wanaongeza "huduma masaa 24".

Inafaa kuandika 'duka la dawa huduma kwa saa 24' ambacho ni Kiswahili sanifu, vilevile, wakati mwingine mgonjwa anasema daktari ameniandikia "madawa mengi" badala ya ameniandikia 'dawa nyingi'. Wapo wanaosema mfanyakazi fulani analipwa 'mahela mengi' badala ya analipwa 'fedha nyingi'.

Haya ni baadhi ya maneno tunayotamka kutokana na mazoea, kadhalika, tuache kuchanganya Kiswahili na Kiingereza au lugha nyingine pasipo ulazima wa kufanya hivyo. Akiwasalimia wasikilizaji wakati wa sikukuu ya "Krismas", kupita chombo kimojawapo cha habari, mtangazaji anasema "twenty twenty-two" inakuja badala ya kusema 'mwaka ishirini ishirini na mbili unakuja'.

Ikumbukwe kwamba Tanzania ni chimbuko la Kiswahili hivyo Watanzania wabadilike wanapozungumza wazingatie uhalisia wake na faida kwa taifa lao. Watu wajitahidi sana kuzingatia Kiswahili sanifu kwa nia njema ya kukuza lugha hiyo kwa maslahi ya taifa.

Kwa upande mwingine, ni fursa kubwa Kiswahili kitakapokuwa lugha rasmi ya mawasiliano duniani taifa litanufaika, hivyo, watangazaji mnapokuwa kwenye "studio" za runinga na redio kuweni makini na kuzingatia matumizi ya Kiswahili sanifu hewani mnapotangaza, kwa kuwa watu wengi wanawasikiliza na wengine kutoka nje kama lugha I mbovu watajifunza nini.

Mathalani, msikilizaji wa nchi za nje, akisikia mtangazaji, amesema bado "lisaa limoja" kumaliza kipindi badala ya kusema bado saa moja kumaliza kipindi atajua "lisaa limoja" ndicho Kiswahili sanifu wakati amepotoshwa.

**INAENDELEA UK.12**

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

# Uhaba, ukosefu intaneti unavyotesa Afrika kimawasiliano kwenye corona

UVIKO-19 umeisumbua dunia kwa miaka karibu mitatu sasa. Lakini kwa mataifa yaliyoendelea mawasiliano bora kiuchumi, kijamii na kwenye nyanja nyingine yameendelea kuimarika kupitia teknolojia ya intaneti.

Mataifa maskini yameendelea kuachwa nyuma, yote hayo ni kutokana na ukosefu wa intaneti na Teknolojia ya Habari na Mwasiliano (TEHAMA).


Wanafunzi kuendelea kusoma kwa furaha na shughuli za uzalishaji viwandani, utoaji huduma na biashara katika mataifa yenye uchumi mkubwa havikutatizika wakati wa corona.

Lakini barani Afrika, taarifa ni tofauti, shule nyingi zilifungwa hata kwa miaka miwili chanzo kikiwa ni ukosefu wa madarasa kwa njia ya mtandao, hakuna intaneti wala namna bora ya kuwaunganisha wanafunzi, walimu, wahadhiri na matini au vipindi waweze kusoma kwa upande wa elimu.

Kadhalika na kwenye miradi ya uzalishaji viwandani, kukosekana mtandao hiyo kumekuwa changamoto kwa mataifa maskini na yenye uchumi unaokua.

Kwa mujibu wa UN NEWS takriban watu bilioni 2.9 duniani hawajawahi kutumia intaneti kati yao zaidi ya bilioni mbili au asilimia 96 wanaishi kwenye nchi zinazoendelea, Ripoti ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa mwishoni mwa mwaka jana inaeleza.

Ni ripoti ya International Telecommunication Union (ITU), inayokadiria kuwa idadi ya wanaotumia mitandao mwaka 2021 iliongezeka hadi kufikia bilioni 4.9 kwa kiasi fulani ikisababishwa na kuunganishwa zaidi kimtandao ili kuukabili UVIKO-19 au "COVID-19 connectivity boost".



Wananchi wakifurahia intaneti mijini. **PICHA: MTANDAO**

> **Tunajitahidi kuona kuwa hakuna anayeachwa katika jukwaa hili la teknolojia na mawasiliano.**

UN NEWS inasema hizo ni taarifa nzuri kwa maendeleo duniani, lakini kwa ITU inaeleza kusikitishwa kuona kwamba uwezo wa watu dunia kuunganishwa kwenye intaneti umebakia kuwa kwenye madaraja, maskini na matajiri.

Ni kwa sababu mamia kwa maelfu ya maskini hawajaweza kutumia intaneti na mitandao ya mawasiliano.

Aidha, wapo wengine ambao wameweza kushirikiana vifaa na miundombinu lakini kama si kwa kushirikiana inamaanisha kuwa wasingeweza kutumia intaneti.

"Licha ya kwamba theluthi mbili ya watu duniani imeunganishwa kwenye mitandao, kuna kazi kubwa zaidi na juhudi nyingi zinahitajika ili kuwaunganisha watu wengi kwenye mtandao wa intaneti," anasema Houlin Zhao, Katibu Mkuu wa ITU.

"ITU itafanyakazi kwa bidii zaidi na wadau wote ili watu bilioni 2.9 waunganishwe. Tunajitahidi kuona kuwa hakuna anayeachwa katika jukwaa hili la teknolojia na mawasiliano."

**ONGEZEKO INTANETI**

Chombo hicho cha UN kinasema ongezeko hilo la idadi ya watu wanaotumia intaneti wakati wa corona linathibitisha kuwa kuimarisha mawasiliano ya mtandaoni ni njia mojawapo iliyotumika kuepusha kusambaa kwa corona.

Taarifa yake inasema kuwa kulikuwa na ongezeko la watumiaji milioni 782 waliojiunga na mitandao ya intaneti kuanzia 2019.

Ongezeko la asilimia 17 ni matokeo ya kuchukua tahadhari za kujikinga na UVIKO -19 kama kuweka karantini, kufunga uzalishaji, kufunga shule na vyuo na mahitaji ya raia wa nchi mbalimbali kwenye huduma za kibenki.

Ripoti ya ITU inasema ongezeko la matumizi ya intaneti liliongezeka kwa asilimia 10 kwa mwaka wa kwanza wa COVID-19 kikiwa ni kiwango kikubwa zaidi katika muongo mmoja.

Hata hivyo, ongezeko hilo halilingani ni la upande mmoja wa mataifa yaliyoendelea kiuchumi.

Upatikanaji wa intaneti siyo rahisi kwa nchi au mataifa maskini ikiwamo Afrika ambako robo tatu ya wananchi wake hawajawahi kutumia mitandao na kwamba nchi 46 zilizo maskini zaidi zikiwa wahusika wakuu.

Doreen Bogdan-Martin, Mkurugenzi wa ITU, ananukuliwa na UN NEWS, akisema "Tofauti kubwa hii ya utumiaji wa intaneti duniani kati ya mataifa yaliyoendelea na maskini ni kubwa. Theluthi moja pekee ya Waafrika ndiyo inayotumia intaneti."

**WAZEE HAWAMO**

Ripoti inaonyesha kwamba vijana, wanaume na wakazi wa mijini na majini hutumia zaidi intaneti kuliko wazee, wanawake wakazi wengi wa vijijini barani Afrika.

Ikizungumzia pengo la kijinsia linaonekana zaidi kwenye mataifa yanayoendelea, kinamama wakibakia nyuma kwenye matumizi ya mitandao hiyo.

Umaskini, ujinga na uhaba wa umeme na kukosekana uelewa na taarifa za matumizi ya vifaa vya kidijitali na TEHAMA maeneo hayo hupunguza matumizi ya intaneti, ITU inabainisha.

## Inashangaza vyombo vya habari vinapoongoza kuboronga Kiswahili

INATOKA UK.11

Mathalani, msikilizaji wa nchi za nje, akisikia mtangazaji, amesema bado "lisaa limoja" kumaliza kipindi badala ya kusema bado saa moja kumaliza kipindi atajua "lisaa limoja" ndicho Kiswahili sanifu wakati amepotoshwa.

Siyo watangazaji tu bali pia hata baadhi ya viongozi wetu wa siasa na madhehebu mbalimbali, nimewasikia wakifanya makosa kama hayo wanapokuwa wakiongea na wananchi (kwenye mikutano) au waumini wao (wakati wa ibada au mikutano).

Kuna mchungaji mmoja akiwa kwenye tukio maalum kanisani alipoona kwenye ratiba imeandikwa mashule hakusita kuwakosoa na akasema "mimi ni mwalimu wa Kiswahili mmekosea siyo 'mashule' bali ni shule".

Anachomaanisha ni kwamba shule haina wingi au "mashule" bali linabaki hivyo hivyo iwe ni shule moja au shule nyingi. Ni vizurikujenga mwelekeo wa kukosoana kwa faida ya wote.

Mambo ya mitaani yabaki hukohuko na kunapokuwa kwenye shughuli za kujenga taifa Kiswahili sanifu kizingatiwe. Matangazo mbalimbali ya biashara yanayorushwa hewani na vyombo vya habari mbalimbali pia yazingatie matumizi ya lugha sanifu.

Mwisho niombe Baraza la Taifa la Kiswahili na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI ) zisaidie kukuza na kuendeleza Kiswahili kwa faida ya taifa ni imani kwamba lugha hiyo itakapokuwa rasmi ya mawasiliano duniani wengi watafaidi kama vyombo vya habari au wafanya kazi za ukalimani hasa Watanzania wenye wepesi kuzungumza na kuzielewa lugha nyingine.

Wanaokipenda Kiswali pamoja na mimi tutaendelea kumshukuru Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere; kwa kukipa kipaumbele hadi kikawa lugha rasmi ya taifa. Kwa taifa lenye makabila zaidi ya 120 kila moja na lugha yake ya asili, kuwa na lugha moja inayounganisha ni mafanikio makubwa.

Sasa wanazungumza na kuelewana bila kikwazo chochote ni jambo la kujivunia, nikiwa mtumishi wa umma nimetembelea maeneo mengi nchini mijini na vijijini na kinachofurahisha, hakuna ambako nimewahi kuulizwa ninatoka kabila gani.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Mwanasheria: Staha ya mama kazini inalindwa na sheria zake

KAMA ilivyo kumiliki ardhi, elimu na masuala ya kisiasa kunavyotajwa kuwa maeneo yenye unyanyasaji kijinsia, unaowasukuma wanawake pembeni na kuwainua wanaume, kadhalika ajira nazo hazijaukwepa mkondo huo.

Wakati wanaume wanapewa kipaumbele kwenye kazi na ajira, kinamama wanawekwa kando au hata wakiajiriwa hupunjwa ujira, kubaguliwa, kufukuzwa kiholela na hata kuonekana mizigo wakiwa wajawazito na wazazi.

Wakidaiwa wanaleta hasara zaidi badala ya tija kwenye kampuni, wanawake ni waathirika wa kazi zisizo na staha au ajira zisizoheshimu haki na stahiki za wafanyakazi.

Kwa mfano zisizo na mikataba, vibarua wa muda mrefu, hawapandishwi madaraja wala mishahara, kulipa ujira kiduchu kwa kazi kubwa, kunyimwa likizo na hata kunyanyaswa kingono.

Kwanini wanawake wanaathirika na kazi zisizo na staha? Ni swali analoulizwa wakili Renata Selemani, kutoka taasisi ya Bright Jamii Initiative ya Dar-es- Salaam, anapozungumza na Nipashe.

Anasema chanzo ni sheria. "Zina upungufu hazitambui majukumu ya nyumbani wala ya kazini ya mwanamke. Mfano linapotokea suala la kupandishwa vyeo na mishahara waajiri wanaangalia utendaji wa mfanyakazi kwa jicho moja kwa wanawake na wanaume bila kujali kinamama wana majukumu tofauti mbali na ya kazini." Anadokeza.

"Mama huyu akitoka ofisini, akifika nyumbani ni mlezi wa familia, mke, mtunza wagonjwa au wazazi, kubeba mimba na uzazi. Tunatakiwa kuongeza uelewa wa masuala ya kijinsia kwa waajiri maana wanawake wana kazi nyingi na ngumu zaidi nyumbani waajiri watazame pia vigezo vya kijinsia kupandisha watumishi mishahara na madaraja," anasema Renata.

Anasema baadhi ya waajiri ukipata ujauzito wameweka wazi unatimuliwa au unakosa nafasi uliyokuwa unaishikilia awali, ikimaanisha hata ujira unapungua, hii si haki.

Wakati mwingine wanawake wana sifa zote, lakini ubaguzi na changamoto za kukosa ajira zinawalazimisha kufanyakazi kwa ujira kiduchu, kuliko kuishi bila kazi, kutokana na changamoto za ugumu wa maisha kama hizo wanafanyakazi ambazo hazina staha.



Kinamama kufanyakazi na watoto mgongoni ni changamoto katika sekta ya kazi. **PICHA: MTANDAO**

> **Kutokana na changamoto hizo wanawake wanafanya kazi zinazowadhalilisha kwa sababu za kuogopa kupoteza kazi ya mshahara mdogo walizonazo.**

Anasema inatokea baadhi ya wawekezaji hawaheshimu sheria za kazi wanawatukana, kuwakataza watu hata kwenda chooni, hawataki wajawazito na wazazi kwa kuogopa uzalishaji utapungua.

"Kutokana na changamoto hizo wanawake wanafanya kazi zinazowadhalilisha kwa sababu za kuogopa kupoteza kazi ya mshahara mdogo walizonazo. Kuna shida ya ajira hivyo ukiendelea kudai haki unatimuliwa."

Ufumbuzi ni nini? Renata anajibu kuwa sheria bora za kazi na zinazoheshimu haki za binadamu na usimamizi wa stahiki za waajiriwa ndilo jibu. Mwajiri anayepuuza sheria afuatiliwe na kuchukuliwa hatua kwa mfano kazi zisizo za kitaaluma ni za wazawa sio wageni, lakini wapo wageni wanafungua na kufunga "mageti" viwandani sheria ziwamulike.

Anawahimiza wanawake wasikae kimya wazungumzie matukio ya uvunjifu wa haki za wafanyakazi watoe taarifa za unyanyasaji mahali pakazi ili kupunguza matukio hayo.

Renata anatoa ushauri maalumu kwa kinamama kuhusiana na kuwapo madai ya kuwanyanyasa watumishi wa ndani na kuwafanyisha kazi sizizo na staha.

"Ukiona kuna mwanamama anaajiri mtoto kuwa mtumishi wa ndani, kumtumikisha kazi za shuruba toa ripoti. Ukiacha mambo yanaendelea na sisi tunakuwa wanyanyasaji wa watoto wanaotufanyia kazi za ndani."

Anawakumbusha wasiwe wepesi kujitetea na kulinda unyanyasaji mfano, zipo taarifa za wasichana kubakwa na wanaume au vijana kwenye nyumba wanapofanyakazi.

"Binti akileta mashtaka ananyanyaswa kina mama wa kwanza kuwashambulia mfano mume wangu akupende una nini? Unamfukuza badala ya kufuatilia mashtaka, kujua ukweli na kutoa msaada. Tusiwe sehemu na wanyanyasaji na kuwashutumu wanaokupa taarifa."

Anawataka wanawake wafanyakazi kufikisha ripoti za unyanyasaji kazini kwa maofisa kazi, wajumbe wa kamati za ulinzi na usalama, dawati la jinsia na polisi ili kuondoa usiri unaowaumiza mahala pa kazi.

Mwanaimani Abdalah, ni mjumbe wa Jukwaa la Wanawake wilayani Mafia (SAWAMA), ameshiriki kwenye utafiti wa kufuatilia uwepo wa kazi zenye staha hotelini, utalii, uvuvi, wahudumu wa baa na wauza migahawa uliodhaminiwa na Shirika la ActionAid, linalodhamini mradi wa kazi zenye staha ukilenga vijana, wilayani humo.

Akizungumzia wanawake anasema: "Wengi hawana mikataba, walio nayo hawana nakala. Wengi wanahofia kubeba mimba hasa sekta ya utalii kwenye msimu wenye wageni wengi. Ukipata mimba umejifukuza kazi." Anasema.

"Utumikishaji wanawake kwa ajira kidogo pia umedhihirika. Kwenye baa hawana mishahara, hutimuliwa kienyeji. Wanatakiwa kuvutia wateja, usipotimiza hilo unafukuzwa kinyemela. Wanaweza kutimua wote na kuletwa wengine kuna maelezo ya "kuingiza bando jipya." Anasema Mwanaimana.

Wanawake wa baa na migahawani hata hotelini huvumilia unyanyaswaji kingono. Hulazimika kufanya ngono na watu wengi, jambo wanalosema linawachosha na kuwadhalilisha, anaongeza.

Akizungumzia maeneo mengine waliyoyafanyia utafiti anataja wafanyakazi kulipwa ujira kiduchu na kazi zisizo na mikataba kwenye kampuni za kuzalisha vifaranga, kufuga, kuvua na kuwafungasha kamba walizozitembelea.

"Wafanyakazi wanalipwa Shilingi 170,000 kwa mwezi bila kujali kiwango cha elimu wala uzoefu, lakini nao hawana mikataba."

**MAFANIKIO**

Mwanaimani anasema baada ya utafiti waliwasilisha ripoti kwa maofisa kazi na serikalini na ufuatiliaji ulifanyika na sasa wafanyakazi wa uvuvi wanapewa mikataba na nakala zake pia risiti ya mshahara "salary slip.'

"Zamani walikuwa wanasaini karatasi za malipo ya mishahara bila kuona kiasi. Kupuuza sheria kunatokana na kukosekana maofisa kazi kufuatilia haki za wafanyakazi kumesababisha ukiukaji wa sheria."

Anasema waligundua baadhi ya wafanyakazi wanakwenda kwa watendaji wa vijiji au kata kulalamikia kunyanyaswa na migogoro kazini, lakini hawapati ufumbuzi kwasababu watendaji hao wanawaeleza waajiri kuhusu malalamiko hivyo wafanyakazi hutimuliwa kiholela.

Änasema kama wangekuwapo maofisa kazi hayo yasingetokea.

Renata na Mwamini na wadau wengine kutoka Bara na Zanzibar wanashiriki mkutano unaoandaliwa na ActionAid Tanzania, kujadili mradi wa kazi zenye staha kwa vijana uliofanyika Desemba mwaka jana.

Katika mapendekezo yao kufikia kazi zenye staha wanashauri itungwe sheria ya kusimamia watumishi wa ndani ili kabla ya kuajiriwa wafike kutoa taarifa kwa viongozi wa serikali za mitaa.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Ni raha tupu ujenzi madarasa mapya Shinyanga kwa heri msongamano



Madarasa mapya yanayojengwa kwa fedha za UVIKO -19 yataanza kutumika wiki ijayo shule zikifunguliwa. **PICHA: MTANDAO**

SERIKALI imepokea mkopo wa Shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) maarufu fedha za UVIKO-19 na kuzielekeza kwenye miradi mbalimbali ukiwamo ujenzi wa madarasa kupunguza uhaba wa miundombinu hiyo kwenye shule za sekondari na msingi.

Katika Manispaa ya Shinyanga fedha za ujenzi wa madarasa ni Sh. milioni 800.8, ukitarajia kujenga madarasa 44, kwenye shule za sekondari 35 na madarasa ya awali ni tisa.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga Jomaary Satura, anasema ujenzi wa madarasa 44 umekamilika kwa asilimia 100 na wanafunzi wanaotarajiwa kuanza shule wiki ijayo watayatumia na hakuna atakayekosa pa kusomea.

"Baada ya kupokea fedha za UVIKO-19, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, tulizisimamia ipasavyo na kuhakikisha azma ya Rais Samia Suluhu Hassan inatimia, ya kumaliza upungufu wa madarasa shuleni," anasema Satura.

Kaimu Ofisa Elimu Shule za Sekondari Manispaa ya Shinyanga, Chibugu Mugini, anasema halmashauri hiyo inatarajia kupokea wanafunzi 3,990 kuingia kidato cha kwanza na wote wataingia kwenye vyumba vya madarasa, na hakuna mwanafunzi ambaye atakosa nafasi.

Anaongeza kuwa fedha hizo zimemaliza tatizo la upungufu wa vyumba hivyo, na kwamba wanafunzi watasoma katika mazingira rafiki na wote 3,990 watakaoingia kidato cha kwanza, hakuna wanafunzi ambao watakosa madarasa au kusubiri uchaguzi wa pili, anasema Mugini.

> **"Uwekaji mazingira mazuri ya wanafunzi kusoma, ni hamasa kubwa ya kufanya vizuri kitaaluma, sababu watakuwa na ari ya kupenda shule na masomo, kutokana na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili.**

Juliana Limbe ni Mkuu wa Sekondari ya Mwawaza katika Manispaa ya Shinyanga, anasema shule hiyo kwa sasa ina madarasa saba, lakini awali ilikuwa na madarasa sita, lakini baada ya kupata fedha za UVIKO-19 Sh. milioni 20 wamefikia idadi hiyo.

Anasema baada ya kuongezeka darasa hilo hakuna upungufu wa vyumba vya madarasa shuleni hapo, na kwamba wana jumla ya wanafunzi 296, ambao kila darasa wanaingia wanafunzi 45 na hakutakuwa na msongamano madarasani na wanafunzi watasoma kwa nafasi na kuelewa vizuri masomo yao.

Marco Msangwa Mkuu wa Sekondari ya Kizumbi, anasema shule hiyo ina wanafunzi 752 na wanatarajia kupokea wengine 352 wanaoingia kidato cha kwanza na shule ina vyumba vya madarasa 14, wakiongeza vingine viwili vilivyojengwa kwa fedha za UVIKO-19 hakutakuwa na upungufu wa vyumba hivyo.

Winfrida John ni mwanafunzi ambaye anasoma kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Mwawaza, anasema ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa utawawezesha kupata elimu bora, sababu watakuwa wakisoma wachache darasani na kuelewa masomo.

"Mnaposoma wanafunzi wengi darasani tena kwa kubanana mnakuwa na kero nyingi inakuwa vigumu kuelewa masomo, mnaona kero, kukosa furaha na uchangamfu lakini mkiwa wachache inaongeza uelewa sababu kutakuwa na mazingira yanayowawezesha kusoma kwa furaha," anasema Winfrida

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Kizumbi, Gambalale Paul, anasema wazazi wanaishukuru serikali na Rais Samia kwa kutoa fedha ili nchi nzima ijenga vyumba vya madarasa ambavyo kutokana na sera ya serikali kugharamia elimu kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi shuleni, tofauti na miaka ya nyuma.

Anasema kutokana na wanafunzi kuwa wengi shuleni, bila kutoa fedha za kujenga madarasa, wanafunzi wangesoma kwa shida kwa kubanana na kusongana kupindukia na wengine wangeingia madarasani kwa awamu.

Anakumbusha kuwa licha ya wazazi kubanana kujenga madarasa, lakini kwa sasa Rais Samia amerahisisha kazi hiyo. "Wazazi tuna mshukuru sana Rais Samia kwa kujenga vyumba hivi vya madarasa sababu watoto wetu wengesoma kwa kubanana darasani, na wengine kukosa hata nafasi, lakini sasa hivi wote watakuwa shuleni tena kwa kuachiana nafasi na hakuna kuambukizana corona,"anasema Paul.

Diwani wa Kata ya Kitangili Manispaa ya Shinyanga, Mariam Nyangaka, anasema ujenzi huo wa vyumba vya madarasa, ni mkombozi kwa wanafunzi kielimu na kuwataka wazazi wawapeleke watoto shule ili waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza wapate elimu.

Anatoa mfano katika Shule ya Sekondari Busulwa iliyoko Kitangili, ina tarajia wanafunzi 182 kujiunga na kidato cha kwanza, lakini wanafunzi ambao wamechukuliwa fomu na wazazi wao ni 129 na kuwahimiza wengine kufanya hivyo.

Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, anasema ujenzi wa vyumba vya madarasa ni chachu kubwa katika suala la elimu, na kueleza kuwa katika fedha za mfuko wa jimbo, ametoa Shilingi milioni 34.2 kuunga mkono juhudi za wananchi kukamilisha maboma ya madarasa ambayo walianzisha kwa nguvu zao.

Katambi ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, anasema uwekaji mazingira mazuri ya wanafunzi kusoma, ni hamasa kubwa ya kufanya vizuri kitaaluma, sababu watakuwa na ari ya kupenda shule na masomo, kutokana na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili.

"Suala la elimu ni muhimu sana katika nchi inayopenda maendeleo, na ndiyo maana serikali ilitafuta fedha na kuzitoa kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa nchi nzima, ili wanafunzi wasome katika mazingira bora, jambo ambalo anahitaji pongezi," anasema Katambi.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anawashukuru wananchi kwa kuunga mkono juhudi za serikali kutatua changamoto za upungufu wa madarasa, kwa kujenga maboma na hata kushiriki kwenye kuchimba msingi.

Anasema suala la utatuzi wa changamoto mbalimbali linawahusu wananchi na kuwataka kushirikiana na serikali, kwa sababu wote wana lengo moja la kufanikiwa, na kuwaomba wasichoke kuendelea kujenga maboma na madarasa kwa nguvu zao wenyewe na serikali itayamalizia ili kuzuia upungufu.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, akiwa mkoani Shinyanga, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote, katika ukusanyaji wa fedha za mapato ya ndani, watenge asilimia 40 na kuzielekeza kwenye kumalizia maboma hayo.



## Mbinu mpya ukeketaji watoto yafichuliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UTUMIAJI wa majivu na kucha ni kati ya mbinu mpya zinazotumiwa na mangariba kufanya vitendo vya ukeketaji kwa watoto.

Ukeketaji ni tendo la kukata sehemu za viungo vya uzazi vya mwanamke.

Aina hii mpya inafanyika kwa siri kubwa wakati wa kuogesha watoto.

Akizungumza jana wakati wa mahojiano na gazeti hili, Mratibu wa Shirika lisilokuwa la Kiserikali la Women Wake Up ((WOWAP), Nasra Suleiman, alisema serikali inafanya juhudi kubwa kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa, lakini mangariba wanabuni mbinu mpya kila wakati.

"Utimiaji wa majivu na kucha umekuwa ni kati ya mbinu bunifu zinazotumiwa na mangariba katika ukeketaji, lakini kuna wakati katika Wilaya ya Chamwino tulipata taarifa ya mangariba kutumia magadi na tumbaku ambapo husugulia sehemu husika kusinyaa kabisa," alisema.

Alisema tatizo la ukeketaji ni janga linaloathiri afya na saikolojia ya watoto wa kike.

"Sisi kama wadau wa watoto tumekuwa tukipinga vitendo hivi kwa kuelimisha jamii na kusaidia kujengea uwezo mifumo ya ulinzi wa mtoto ili waweze kushughulikia masuala haya kwa mitazamo ya kisera na sheria za nchi pamoja na juhudi kubwa tunazofanya wananchi ambao wamekuwa wakiabudu mila na desturi zinazoambatana na ukeketaji wamekuwa wakibuni mbinu mpya za kuendeleza mila hii na imekuwa vigumu kuwanusuru watoto wengi na ukatili huu," alisema.

Mratibu huyo alisema suala la mila na desturi pamoja na uelewa mdogo wa wananchi katika haki za watoto mbinu mpya wanazobuni ni kati ya changamoto za kukabiliana na ukatili huo.

Alisema pamoja na changamoto zote, kuna kundi la jamii ambalo limeweza kuelimika na kuendelea kusaidia kuelimisha wenzao kuachana na mila hiyo.

# Watoto wenye ulemavu waomba wazazi waelimishwe

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

WATOTO wenye ulemavu katika wilaya za Bahi na Mpwapwa, wamewaomba wafadhili wanaotoa misaada kwa ajili yao, kutoa elimu kwa wazazi kuacha tabia ya kuwaficha majumbani badala ya kupeleka shule.

Ushauri huo ulitolewa na watoto hao kwa nyakati tofauti walipokuwa wakizungumza kwenye kikao cha pamoja kati yao, wazazi na wafadhili wa mradi wa MyRight, kilichofanyika juzi katika kijijini Nh'gome wilayani Bahi.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Annamaria Daud (10) mwenye ualbino na mwanafunzi wa darasa la pili shule ya msingi wasioona Buigiri, alisema wafadhili pamoja na kutoa misaada mbalimbali kwa watu wenye ulemavu, wanashauriwa kuwaelimisha wazazi kuacha kuwaficha watoto majumbani na kusababisha kuleta umaskini kwenye familia zao.

Annamaria alisema bado kuna watoto wengi vijijini wanaotakiwa kupelekwa shule na kupatiwa huduma za kiafya, lakini wamefichwa na wazazi wao majumbani kutokana na uelewa mdogo.

"Tunawaomba hawa wafadhili wetu pamoja na misaada yao pia waelekeze elimu zaidi kwa wazazi ambao wana watoto wenye ulemavu, lakini wamewafungia majumbani badala ya kuwasomesha ili waweze kuondokana na umaskini," alisema Annamaria.

Naye Egra Hamisi, mwanafunzi wa darasa la nne katika shule hiyo alisema kuna asilimia kubwa ya watoto wenye ulemavu wanaofichwa na kunyanyaswa na familia na kusababisha kukosa haki zao za msingi.

Alisema pamoja na juhudi za serikali za kutaka watoto wenye ulemavu kupata elimu na huduma zingine, kuna kila sababu wafadhili wakazielimisha familia hizo ili waachane na tabia ya kuwaficha.

Mratibu Mkuu wa mradi Myright, Emmanuel Mhehwa, alisema mradi umekuwa ukifanya kazi zake za kuhudumia watoto kwa kushirikiana na Chama cha Wasioona Tanzania (TLB) Jumuiya ya Wasioona Zanzibar (ZANAB) na Chama cha Watu wenye Ualbino (TAS).

Mhehwa, alisema lengo ni kuhakikisha kuwafikia watoto wenye ulemavu majumbani kwa ajili ya kuwadahili ili kuwawezesha kupata huduma mbalimbali ikiwamo ya elimu na afya.

Alisema mradi huo kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi 2021 umefanikiwa kuwafikia watoto 344 kwa mikoa miwili ya Singida na Dodoma ambao wamedahiliwa na kupata huduma za msingi ya afya na elimu na mahitaji mengine.



Wageni waalikwa na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama wakiwa katika hafla ya kuwaapisha baadhi ya mawaziri, manaibu waziri na makatibu wakuu Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kamera kufungwa kunasa wanaogonga wanafunzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na idadi kubwa ya wanafunzi kugongwa na magari na kupoteza maisha katika Barabara kuu ya Dodoma - Dar es Salaam, Halmashauri ya Chamwino inapanga kufunga kamera katika eneo la Buigiri kwa ajili ya kunasa magari yanayopita kwa mwendo kasi.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chamwino, Kenneth Yindi, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma wakati akizindua vyumba vya madarasa yaliyojengwa kwa fedha za UVIKO-19, katika Shule ya Sekondari wa Buigiri.

Yindi, alisema kata hiyo ina shule sita na barabara kuu imepita katika vijiji vitatu.

"Wanafunzi wengi wanagongwa, magari yanakimbia sana hasa yale ya serikali, wanafunzi na hata wananchi wanapoteza maisha kutokana na ajali za barabarani," alisema Yindi.

Aidha, alisema alitembelea maeneo mbalimbali nchini yaliyopitiwa na barabara kuu ili kutafuta njia za kuepukana na ajali hizo.

"Tumeshafanya kikao na kamanda wa kikosi cha usalama barabarani na kupeleka ombi rasmi kwa kutumia wataalamu wa ICT tutafunga kamera nne," alisema. Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema suala la kufungwa kamera ni jambo zuri kwa kuwa litasaidia kuokoa maisha ya wanafunzi katika shule hizo pamoja na watu wote wanaoitumia barabara hiyo.

"Fungeni hizo kamera huenda tukapata suluhisho la ajali ambazo zimekuwa zikijitokea katika eneo hili mara kwa mara na kukatisha uhai wa vijana wetu," alisema.

Kadhalika, alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya na vyombo vya ulinzi na usalama kutafuta suluhisho la haraka.

Akipokea taarifa ya ujenzi wa madarasa, Buigiri Sekondari ilipokea jumla ya Sh. milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa matatu na ofisi ya walimu.

Ofisa Elimu Mkoa wa Dodoma, Gift Kyando, alisema ujenzi wa madarasa umekamilika na ifikapo Januari 17 watoto wote watakuwa wameripoti shuleni. Alisema watafanya kampeni kuhakikisha watoto wanaripoti shuleni bila kuwa na visingizio vya kukosa sare, madaftari na mahitaji mengine ili kazi ya kufundisha ianze mara moja.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Pili Mbanga, alisema chama hicho kinawashukuru wote waliohakikisha ujenzi unakamilika kwa wakati.



# Radi ilivyoua wanne wakichimba kaburi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WATU wanne wamefariki dunia na mmoja kujeruhiwa baada ya kupigwa na radi walipokuwa wakichimba kaburi la ndugu yao katika Kijiji cha Kibaoni, Wilaya ya Chunya.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, aliwataja waliofariki kuwa ni Yohana James (30), mkazi wa Majengo, Paul Mwasongole (40), mkazi wa Chunya Mjini, Swalehe Ibrahim (23) mkazi wa Chunya Mjini na Bonny Lauliano kutoka mkoani Songwe na majeruhi Zuberi Mahona (40).

Alisema tukio hilo lilitokea Januari 9, saa saba mchana katika makaburi ya eneo la Kibaoni wilayani Chunya.

"Radi hiyo iliwapiga wakiwa wanachimba kaburi kwa ajili ya kuhifadhi mwili," alisema Mayeka.

Alisema miili yao imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Chunya na majeruhi anaendelea kupatiwa matibabu huku akiwaomba wananchi kuendelea kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha msimu wa mvua inayoambatana na radi.

Miongoni mwa mashuhuda wa janga hilo, Meshack Luvanda aliyekuwapo eneo la tukio, alisema alikuwa miongoni mwa walioshikiri uchimbaji kaburi.

Alisema eneo hilo lilinyesha mvua kubwa iliyoambatana na radi lakini kutokana shughuli za mazishi za ndugu yao walilazimika kuendelea na uchimbaji wa kaburi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kijiji cha Kibaoni, Joshua Mlambala, alisema radi iliyoambatana na mvua kubwa ilipiga eneo lililokuwa linachimbwa kaburi na watu hao walijificha katika miti na majeruhi alikuwa kaburini akichimba.

Kwa siku nne mfululizo baadhi ya maeneo mkoani Mbeya mvua kubwa iliyoambatana na radi ilipiga na kusababisha athari mbalimbali ikiwamo mafuriko na baadhi ya vibanda vya biashara kuungua eneo la Airport ya zamani.



Kiongozi wa timu ya kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19 kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Subisya Kabuje (kushoto), akimkabidhi vipeperushi vya kuhamasisha chanjo Mratibu wa Chanjo Mkoa wa Songwe, Dk. Enock Mwambalaswa, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## W'biashara walilia miundombinu bora ya soko

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Forest, wameuomba uongozi wa soko hilo, kuwatengenezea miundombinu ya soko ili wafanye biashara katika mazingira mazuri.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wafanyabiashara wa soko hilo walisema mvua inayoendelea kunyesha imeharibu miundombinu ya soko hilo na kusababisha wateja kutofika maeneo hayo.

Miongoni mwa wafanyabiashara hao, Yasinta Abbas, alisema kipindi hiki cha mvua, barabara ndani ya soko hilo hazipitiki hali inayosababisha wateja kushindwa kufika maeneo hayo na kusababisha ukata na bidhaa zao kuharibika.

Alisema soko hilo pia halina choo hali inayosababisha kutumia umbali mrefu kwenda kufuata huduma maeneo mengine.

"Serikali ilijenga soko hili muda mrefu sana, lakini tatizo ni kwamba hakuna miundombinu rafiki kwa ajili ya kufanyia biashara zetu, wateja wanatukimbia kwa sababu ya mazingira na mbaya zaidi hatuna hata choo tunaomba mtusaidie," alisema Abbas.

Mwenyekiti wa Soko la Forest, Jackson Kamotola, alikiri kuwapo kwa ubovu wa miundombinu katika soko hilo na kwamba licha ya vizimba na majengo, hali ya biashara hairidhishi.

Alisema wajasiriamali na wateja sio wengi kutokana na jiografia ya eneo hilo na wanaendelea kuiomba serikali kuboresha miundombinu ya majengo na vyoo ili kuwavutia wawekezaji na wateja.

Soko hilo linakabiliwa na uhaba wa wafanyabiashara kutokana na miundombinu mibovu na kusababisha kukosa wateja.

# Shirika la SIDO kutengeneza mashine za kisasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KARAKANA ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO), imesema imedhamiria kutengeneza mashine za kisasa ili kukuza uchumi na kuondokana na tatizo la ajira.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa SIDO mikoa ya Mbeya na Songwe, Henerick Mdede alisema wamejipanga kuhakikisha mwaka 2022 kuwa wa mapinduzi makubwa kwa sekta ya viwanda inakuwa na tija wa wajasiriamali.

"Miongoni mwa shughuli tunazokusudia kwa mwaka huu ni uanzishwaji wa viwanda vidogo katika ngazi ya mkoa ili maendeleo ya teknolojia na huduma za ufundi yazidi kushika kasi," alisema Mdede.

Alisema SIDO Mkoa wa Mbeya inamiliki karakana kubwa ambayo inabuni na kutengeneza mashine mbalimbali na kwa mwaka jana walifanikiwa kutengeneza zisizopungua 130 ambayo ilienda kusaidia kwenye uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Kwa upande wake Mratibu wa karakana ya SIDO, Mhandisi Cosmas Kinasa, alisema karakana inaendelea kubuni mashine mbalimbali na kwa sasa mashine 58 zipo sokoni zenye uwezo wa kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Mhandisi Kinasa alisema mashine za kusaga unga zipo za aina mbili zinauzwa Sh. milioni 56 na mahindi yanachakatwa kwa mtindo wa kisasa na mashine za kuchakata mafuta ya alizeti.

SIDO hutoa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo inayowawezesha wananchi kuifikia azma ya serikali ya kuwa Tanzania ya viwanda kutokana na upatikanaji wa umeme vijijini.

Baadhi ya wajasiriamali waliomba SIDO kuuza mashine za kuchakata mazao kwa bei nafuu wanayoweza kuimudu.



## Ruksa kusajili meli za kigeni kupeperusha bendera ya TZ

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Rahma Kassim Ali, amesema Zanzibar sasa rukhusa kufanya usajili wa meli za kigeni zitakazopeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuzuiliwa kufanya hivyo kwa zaidi ya miaka mitatu.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya wizara hiyo katika miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar, waziri huyo ameipongeza serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa juhudi zake wa kulipatia ufumbuzi suala hilo kwa pande mbili kukaa pamoja na kuwasilisha changamoto zilizokuwapo awali.

Alisema kuruhusiwa kwa Zanzibar kusajili meli za kigeni kutatoa nafasi nyingine ya kujipanga na kuzifanyia kazi changamoto zilizojitokeza awali ambazo zilikuwa kikwazo katika utekelezaji wa majukumu.

Alisema baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuingia madarakani alitaka kupatiwa maelezo kamili ya tatizo hilo ikiwamo sababu za Zanzibar kusitishwa kufanya usajili wa meli za kigeni.

Alisema baada ya kupata maelezo hayo alifanya mawasiliano na upande wa pili wa muungano na hatimaye kuruhusiwa kufanya usajili wa meli za kigeni.

Alisema tayari Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA) ambayo ndiyo yenye jukumu la kufanya usajili wa meli za nje, imejipanga vizuri kuhakikisha inatekeleza jukumu hilo kikamilifu na kuepuka kasoro zinazoweza kujitokeza.

Alisema kitendo cha Zanzibar kuzuiliwa kufanya usajili wa meli za kigeni imekosa mapato ya zaidi ya Shilingi bilioni tatu katika kipindi hicho.

"Mamlaka ya Usafiri wa Baharini (ZMA) tayari wamejipanga vizuri kwa ajili ya kuanza usajili wa meli za kigeni na kuzipatia ufumbuzi changamoto zote ambazo zilikuwa kikwazo katika utekelezaji wa majukumu na kusababisha zoezi hilo kukwama," alisema.

Zanzibar ilizuiliwa kufanya usajili wa meli za kigeni baada ya kubainika kwamba meli zilizokuwa zikipeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano kujitokeza kwa kasoro nyingi ikiwamo meli kubeba dawa za kulevya na kujihusisha na vitendo vya uharamia.

Hatua hiyo ilisababisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusitisha jukumu la usajili wa meli za kigeni kwa Zanzibar hadi changamoto na mazungumzo ya kina kufanyika na kuzipatia ufumbuzi kasoro hizo.

# Jengo la maabara kuimarisha uwezo wa kiutendaji Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUKAMILIKA kwa jengo la ofisi na maabara za taasisi ya viwango mjini hapa kutasaidia kuimarisha uwezo wa kiutendaji na kutoa huduma bora kwa watumiaji wa bidhaa, wazalishaji na wafanyabiashara.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema hayo katika sherehe za ufunguzi wa ofisi na maabara za taasisi ya viwango Maruhubi, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Hemed alisema kuwa, serikali ina mpango madhubuti wa kuhakikisha wananchi wake wanatumia bidhaa zilizo bora kwa lengo la kutunza afya zao na mustakabali wa maisha yao.

Alisema, kupitia Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), serikali itaendelea na hatua za kudhibiti ubora wa bidhaa zinazotengenezwa au kuingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

"Serikali itaendelea kuhakikisha upatikanaji bidhaa bora na zenye kukidhi viwango ili kuendana na soko la dunia pamoja na kumlinda mtumiaji," alisema Hemed.

Aidha, aliwataka viongozi na watendaji wa Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), kupima sampuli za bidhaa zote pamoja na kutoa majibu kwa wakati na kuwa makini katika kufanya ukaguzi na udhibiti wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwa kutumia maabara hizo kwa kuwatumia wataalamu wa ndani.

Aliwakumbusha watendaji wa ZBS kufanya kazi kwa bidii, ubunifu, uaminifu na kujiamini katika kusimamia majukumu ya kazi zao.

"Nawaombeni sana mtekeleze vyema majukumu yenu kwani kufanya hivyo mtaimarisha soko la hapa nchini na kuwasaidia wazalishaji wetu wa ndani wakiwamo wajasiriamali kuyafikia masoko ya nje ya nchi," alisema Makamu wa Pili wa Rais.

Pia aliwataka wafanyabiashara kushirikiana na ZBS ili bidhaa zinazoingizwa katika soko la Zanzibar zikidhi matakwa ya viwango husika kwa lengo la kulinda afya na usalama wa mtumiaji.

Naye Waziri wa Biashara Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaabani, alisema nia na azma ya Serikali ya Zanzibar ni kuhakikisha inatoa huduma bora kwa wananchi na ZBS ina mpango wa kufanya mageuzi makubwa katika masuala ya ukaguzi na vipimo kwa bidhaa.

Alifafanua kwamba ndani ya kipindi cha muda mfupi ZBS imeshirikiana na taasisi za tofauti za viwango katika ukanda wa Afrika Mashariki.



Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuberi Ali Malud, akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi katika hanga la askari wa Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) Wete, Pemba. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Shamra shamra za Mapinduzi zazindua madarasa 4

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema kuongezeka kwa idadi ya mahitaji ya elimu kumesababisha serikali kuongeza majengo ya utoaji elimu ili kukidhi mahitaji.

Akifungua madarasa manne katika Shule ya Kiomba Mvua, Mkoa wa Kaskazini Unguja ikiwa ni shamrashamra za miaka 58 ya Mapinduzi, alisema hatua hiyo imelenga kuweka mazingira bora kwa wanafunzi ili wasome vizuri. Alisema ujenzi wa madarasa hayo ni kielelezo cha utekelezaji wa dhamira ya Mapinduzi katika kuona wanafunzi wanapata haki yao ya msingi ya kupatiwa elimu bure.

Waziri Mazrui alisisitiza umuhimu wa wazazi kusimamia na kufuatilia masomo ya watoto wao ili lengo la serikali kutoa wataalamu katika sekta mbalimbali linafikiwa.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis Juma, aliwataka wananchi wanaozunguka eneo la shule hiyo kuwa na nguvu ya pamoja kulinda eneo la shule ili lisivamiwe kwa shughuli zingine za kijamii.

Aliahidi kujenga vyoo vipya na madarasa mengine katika kipindi kifupi kijacho ili kuepusha wanafunzi kufuatia huduma hizo nje ya eneo la shule.

Akisoma risala kwa niaba ya uongozi wa shule hiyo, Mwalim Fauzia Ussi, aliiomba serikali kupitia Wizara ya Elimu, kuwaongezea madarasa pamoja na kuwawekea uzio ili kulinda eneo lao dhidi ya uvamizi pamoja na usalama wa mali za shule.

Zaidi ya Sh. milioni 60 zimetumika katika ujenzi wa madarasa hayo ikiwa ni nguvu za wananchi na viongozi wao pamoja na wizara.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA VYETI



**ABIGAIL SAMUEL KIWELU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0239-0001** kilichotolewa na **ST. FRANCIS GIRLS' SEKONDARI** mwaka **2002.** Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1197-0501** kilichotolewa na **GREEN ACRES SEKONDARI** mwaka **2006.** Cheti cha Chuo **(BACHELOR)** chenye namba BD.SW 0000370 kilichotolewa na **INSTITUTE OF SOCIAL WORK** mwaka **2010.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/12328/2022.**

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

VIGWAZA DRY PORT COMPANY LIMITED
Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya VIGWAZA DRY PORT COMPANY LIMITED yenye namba ya usajili 116892 iliyopo Kata ya Vigwaza Wilaya ya Chalinze Mkoa wa Pwani, iliyosajiliwa tarehe 23/04/2015, wameamua kwa hiyari yao kuifunga Kampuni hiyo kutokana na eneo la Vigwaza kutumika kwa ajili ya shughuli za Bandari kavu. Pia Kampuni inaifunga TIN number 127-032-572 ya Kampuni hii kwa kuwa itakuwa haitumiki tena.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

EDGAR WALTER MASUNYA
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T739 CZS Engine no 2kd1593915
Chassis no kdh2000014920
Imesajaliwa kwa jina la SED ADVENTURES TOURS and SAFARIS
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Taarifa ya polisi
ARU/MUR/RB 11873/2022.

---

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 220/2021**
**Jina la mdai: REMIGIUS SELESTINE BAFULUKI**
**Jina la mdaiwa: FRIDA MICHAEL ASEY**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: FRIDA MICHAEL ASEY**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**
**KUJIBU MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 1 Mwezi wa 2 Mwaka 2022 saa 3:00 asubuhi/mchana kwa mujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 4 Mwezi wa 1 Mwaka 2022.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KITUO JUMUISHI
HUDUMA ZA KIMAHAKAMA
MIRATHI NA NDOA
DAR ES SALAAM

## KUPOTEA KWA OFFER YA KUMILIKI ARDHI

Offer ya kiwanja Na.212 Kitalu 'Q' Kangaye

**Mmiliki aliyeandikishwa:** SEIF HILAL RIYAMI wa S.L.P 2779, Mwanza.

**Muombaji:** KHAMIS RIYAMI wa S.L.P 2779, Mwanza.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba offer ya mmiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea, na ninakusudia kutoa offer mpya badala yake iwapo hakuna pingamizi lolote kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii.
Endapo offer hii ikionekana irudishwe Manispaa ya Ilemela S.L.P 735, Mwanza.

**D.S.Tongora**
**KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA ILEMELA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**Wilaya ya Morogoro Kituo cha Mjini**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi..1..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU :ISSA RASHIDI CHIWANGA WA KICHANGANI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA ZUBEDA ISSA RASHIDI**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 17/01/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 10/01/2022**

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 4/2022**
**Katika Shauri la Mirathi ya RAMADHANI SULEMANI SAIDI…………MAREHEMU**
**Wa NJOMBE**
**Katika shauri la maombi ya kumteua Msimamizi yaliyoletwa na**
**MATHA D/O BAHATI MAYALA………………..Mwombaji**
**TANGAZO KWA UMMA**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi wa 01 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu. Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 10 Mwezi wa 01 Mwaka 2022.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 195 of 2021**
**In the matter of the Estate of the late of the late PAUL GERALD KYAMBA of K/NDEGE within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by PENDO PAUL KYAMBA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 26 day of 01,2022
Dated at Dodoma this 05 day of 01, 2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**Wilaya ya Morogoro Kituo cha Mjini**
**Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi Na..2..2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU :RAJABU ATHUMANI KIDULI - SABASABA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA KASSIM RAJABU KIDULI**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 16/02/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 10/01/2022

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Mvua ya saa 24 yaua watano Msumbiji

**Maputo,** MSUMBIJI

WATU watano wamefariki dunia na wengine 15 kujeruhiwa vibaya, baada ya mvua kubwa kunyesha na kuambatana na upepo mkali, ngurumo na radi vilivyoacha uharibifu mkubwa katika Jimbo la Kusini mwa Msumbiji la Gaza.

"Waliofariki walipigwa na radi," alisema Bonifacio Cardoso, Msemaji wa Taasisi ya Kitaifa ya Hatari za Majanga na Udhibiti, wake katika eneo hilo.

Aliwataka watu kuchukua hatua za tahadhari, ikiwa ni pamoja na kubaki ndani ya nyumba zao wakati wa ngurumo na radi.

Mvua kubwa ambayo ilidumu kwa saa 24, mwishoni mwa juma pia iliharibu nyumba 5,000 na vituo sita vya afya vilizama kwenye maji.

Inakadiriwa kuwa zaidi ya watu 394,000 wameathirirwa na mafuriko katika mvua ya hivi karibuni na msimu wa mvua hadi kufikia Machi, mwaka huu.

Shirika la Majanga la Msumbiji, tayari limekwishapeleka maofisa wake katika eneo hilo, maboti, chakula, mahema na mablanketi, ili kujiandaa kwa mafuriko yanayotarajiwa. **BBC**

## Viongozi Somalia wakubaliana uchaguzi

**Mogadishu,** SOMALIA

VIONGOZI wa kisiasa wa Somalia, wamesema kwamba, wamefikia makubaliano ya kukamilisha uchaguzi wa bunge kufikia Februari 25, mwaka huu, baada ya kuchelewesha kwa muda na kutishia udhabiti wa taifa hilo, lililotatizika kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AFP, hatua hiyo imefikiwa baada ya mashauriano ya siku kadhaa, yakiongozwa na Waziri Mkuu, Hussein Roble na kuhudhuriwa na viongozi wa majimbo.

Taarifa iliyotolewa baada ya vikao hivyo, ilisema kwamba uchaguzi unaoendelea wa bunge la chini, utafanyika kati ya Januari 15 na Februari 25, mwaka huu.

Roble na Rais Mohamed Abdullahi Mohamed au kwa jina lingine Farmajo, wamekuwa wakijibizana kutokana na kucheleweshwa kwa zoezi hilo, hali iliyozua wasiwasi wa kutokea kwa ghasia.

Mwezi uliopita, Farmajo alimsimamisha kazi Roble ingawa yeye mwenyewe ndiye aliyemteua kuwa waziri mkuu, Septemba mwaka 2020.

Jumuiya ya kimataifa, ilikuwa imeelezea wasiwasi wake kutokana na migogoro ya kisiasa nchini humo, wakati kukiwa na changamoto ya makundi ya kiislamu kama vile Al Shabaab, miongoni mwa mengine. **VOA**

# Uganda yafungua shule baada miezi 24

**Kampala,** UGANDA

SHULE zimefunguliwa tena jana ikiwa ni takribani miaka miwili tangu kuanza kwa janga la corona duniani.

Kufungwa kwa shule Uganda, ni mojawapo ya hatua zilizochukua muda mrefu zaidi duniani, tangu virusi hivyo vilazimishe serikali kufunga taasisi za masomo Machi mwaka 2020.

Serikali ya Uganda, ilichukua hatua hiyo mwaka 2020, kwa kufunga shule zote, masoko na mijumuiko ya umma kama mojawapo ya njia za kuzuia kuenea kwa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19.

Rais Yoweri Museveni, alihutubia taifa kuhusu tishio la mlipuko wa virusi hatari vya Covid-19 akiwa kwenye Ikulu ya Entebbe, mwaka huo.

Aliamrisha taasisi za elimu zote, ikiwamo vyuo vikuu kufunga kwa kipindi cha mwezi mmoja, kuanzia Ijumaa ya Machi 20, mwaka 2020.

Pia alibana mikutano ya kisiasa na kijamii, kufungua maeneo ya ibada, hoteli, baa, klabu za muziki na masoko.

Tofauti na taasisi za elimu, agizo la rais alilolitoa mwaka huo, kuhusu mijumuiko hiyo, lilianza kutekelezwa baada ya hotuba yake.

Rais Museveni, alisema hatua ya kufunga shule ililenga kuhakikisha kwamba wanafunzi wanarejea majumbani kwao kabla ya kisa chochote kuripotiwa, ili kuepuka gharama na changamoto za kutafuta wanaoshukiwa kuambukizwa ikiwa kisa kitapatikana na kuwatawanya.

Kuhusu usafiri wa ndege kutoka Uganda kuelekea katika nchi ambako virusi vya Covid-19 vilisambaa sana ikiwamo Ufaransa, Italia, Japan, Hispania, Korea Kusini na China, zilisitishwa safari.

Aliagiza Waganda wote wanaorejea nyumbani kutoka nje watawekwa karantini ya lazima kwa siku 14 pindi wanapowasili kwenye uwanja wa ndege.

Rais Museveni aliwahimiza wananchi kuzingatia maelekezo ya Wizara ya Afya na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Aliisitiza suala la usafi na kushirikiana na wahudumu wa afya, kuripoti kisa chochote kinachoshukiwa kuwa ni cha Covid-19 mapema iwezekanavyo.

Baada ya agizo hilo la rais miaka miwili sasa, nchi hiyo imefungua shule zake. **BBC**



Wanafunzi wakiwa darasani baada ya shule kufunguliwa nchini Uganda, jana. **PICHA: BBC**

# Watoto 9 kati ya 20 wafa moto Marekani

**New York,** MAREKANI

WATU 19 wakiwamo watoto 9 wamekufa kutokana na moto kwenye kitongoji ya Bronx, mjini New York, ukiwa mkasa ulioelezewa kuwa mbaya zaidi na Mkuu wa Zimamoto, mjini humo katika miaka ya karibuni. Mshauri Mkuu wa Meya New York, Eric Adams, Jumapili alihibitisha vifo hivyo wakati ofisa mmoja wa jiji ambaye hakuruhusiwa kuzungumza hadharani, akithibitisha vifo vya watoto.

Dazeni ya watu pia wanasemekana kujeruhiwa wakati wa moto huo, 13 miongoni mwao wakisemekana kuwa katika hali mahututi.

Idara ya Moto New York, ilisema kwamba, zaidi ya wazimamoto 200 walishiriki kuzima moto huo kwenye nyumba za makazi za Twin Park.

Mkuu wa Idara ya Zimamoto New York Daniel Nigro, wakati akizungumza na wanahabari, alisema kwamba wazimamoto walipata watu waliokufa katika kila ghorofa la jengo hilo, lenye ghorofa 19, wengi wakisemekana kuangamizwa na moshi mkali.

Nigro, alilinganisha mkasa huo na ule wa mwaka 1990, kwenye klabu cha Happy Land, ambao uliua watu 87 baada ya mmoja wa wateja kuwasha moto, kutokana na kufukuzwa kwenye klabu hiyo, kufuatia majibizano na mpenzi wake. **VOA**

# KIBOKO WA YANGA KOMBE LA MAPINDUZI ATUA PRISONS

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA Hussein Abel Thomas (pichani) aliyekuwa mchezaji bora kwenye mechi kati ya Yanga dhidi ya Taifa Jang'ombe Jumatano iliyopita katika mechi ya Kombe la Mapinduzi, amesajiliwa na Tanzania Prisons.

**Kipa huyo aliyekuwa kikwazo kikubwa kwa wachezaji wa Yanga, licha ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0, amesajiliwa haraka na timu hiyo ambayo kwa sasa maskani yake yako mkoani Sumbawanga.**

Kwenye mtandao wao wa instagram, Prisons imechapisha picha ya mchezaji huyo na kutoa taarifa ya kumsajili, pamoja na kumkaribisha mchezaji huyo.

"Karibu karibu kipa mwenye hadhi yake, Hussein Abel Thomas ambaye unakuja kuleta kitu kipya kwenye ligi yetu. Sura yako si ngeni kwa Tanzania kwani walikuona ukiwa mchezaji bora katika mechi kati ya Taifa Jang'ombe dhidi ya Yanga kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi msimu huu kule Visiwani Zanzibar na waliouona uwezo wako katika milingoni mitatu," uliandika mtandao huo wa Prisons na kuongeza.

"Hujaja hapa kwa kuwa ulikuwa mchezaji bora wa ile mechi, hapana, ila umekuja hapa kwa uwezo wako tangu ulipokuwa Coastal Union, kuanzia timu ya vijana chini ya miaka 20, timu ya wakubwa na huko ulikotokea kwa sasa Taifa Jang'ombe."

Michuano ya Kombe la Mapinduzi imekuwa ya kuonekana na kujiuza kwa wachezaji wa Zanzibar ambao wengi wao wameonekana kuwa na vipaji vikubwa vilivyofichika.

Kipa huyo anakuwa ni mchezaji wa tatu kusajiliwa na Prisons kipindi hiki cha dirisha dogo, kwani tayari ina saini za mastraika wawili, Aboubakar Malika na Mudathir Said.




NIMETUSUA...




Mshindi wa Bonasi ya Jackpot ya SportPesa, Edgar Gabriel Mlelwa kutoka Mji Mwema mkoani Njombe akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 9. 12 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot inayoshindaniwa wiki hii ni 823,998,440/-. **PICHA: SPORTPESA**

## Chanongo aibukia Ruvu Shooting

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa zamani wa klabu ya Simba na baadaye Mtibwa Sugar, ameibukia Klabu ya Ruvu Shooting, baada ya kutangazwa kusajiliwa akiwa mchezaji huru.

Chanongo, ambaye ni zao la kikosi cha pili cha Simba, amesajiliwa na klabu hiyo kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, wakati timu nyingi kwa sasa zipo kwenye harakati za kuimarisha vikosi vyao.

"Baada ya kugombaniwa sana na klabu kubwa nje na ndani ya nchi, Haruna Athumani Chanongo rasmi amejiunga na timu bora kabisa," imeeleza klabu ya Ruvu Shooting.

Chanongo alipandishwa kukichezea kikosi cha kwanza cha Simba mwaka 2012 mpaka 2015 alipoihamia Stand United na kukaa kwa mwaka mmoja, kabla ya kujiunga na Mtibwa Sugar 2017.

Kwa sasa alikuwa mchezaji huru.

Mbali na mchezaji huyo, Ruvu Shooting pia imetangaza kumsajili kipa wa zamani wa Yanga na Kagera Sugar, akitokea Geita Gold, Benedict Tinoko, lakini ikimsajili Hussein Suleiman 'Chuse' na mchezaji kutoka Zanzibar Abalkassim Suleiman.

## JKT Queens yatuma ujumbe Simba, Yanga

**Na Sada Akida,** ZANZIBAR

KOCHA wa Klabu ya JKT Queens, Ibrahimu Mohamed, amesema huu ni msimu wa mwisho kwao kukosa ubingwa na kuanzia msimu ujao wanarejesha utawala wao wa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ibrahim alisema Simba na Yanga ambazo kwa misimu hii miwili zimekuwa zikipata alama tatu kwenye mgongo wake, wajiandae kupigwa kwani watakuja na sura mpya msimu ujao.

Alisema kwa sasa wanatengeneza timu ya ushindani ili kuweza kurudi kwenye zama zao za kushinda kila mchezo na kutwaa ubingwa.

"Wakae tayari kwa sababu msimu ujao, tunarudisha heshima yetu iliyopotea kwa misimu miwili kwenda watatu, tunatengeneza timu na kurudisha majembe yetu yaliyopotea," alisema Ibrahim.

JKT Queens ambao ni mabingwa mara mbili wa ligi hiyo, wanashika nafasi ya tano kwenye msimamo wakiwa na pointi saba, wakicheza mechi nne na kushinda mbili, sare moja na kupoteza moja.

## ZISIKUPITE

### NDOMBELE KUONDOKA SPURS

MCHEZAJI aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi, Tanguy Ndombele, 25, ana matumaini ya kuondoka Tottenham Hotspur mwezi huu. ***(The Athletic)***

### BERGWIJN ATAKIWA AJAX

WINGA wa Uholanzi, Steven Bergwijn, 24, anaonekana kukaribia kuondoka Tottenhma Hotspurs, huku Ajax ikiwa miongoni mwa timu zinazomwania mchezaji huyo. ***(Fabrizio Romano on Twitter)***

### MBAPPE KUBAKI PSG

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 23, bado anaweza kukataa kuhamia Real Madrid na kusaini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(Le Parisien)***

### SCHICK KUBAKI LEVERKUSEN

MSHAMBULIAJI wa Bayer Leverkusen na Jamhuri ya Czech, Patrik Schick, 25, amesema ana furaha katika klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, licha ya uvumi kuhusu kuhama Januari hii. ***(Bild)***

### DIGNE KUTUA ASTON VILLA

KLABU ya Aston Villa ipo katika mazungumzo ya juu zaidi kumsajili, Lucas Digne, 28, kutoka Everton, huku beki huyo wa kushoto wa Ufaransa akiaminika kupendelea kuhamia kikosi cha Steven Gerrard. ***(Sky Sports)***

### NEWCASTLE YAMTAKA WOOD

NEWCASTLE United imewasiliana na Burnley kumnunua mshambuliaji wa New Zealand, Chris Wood, 30. ***(Telegraph)***

### OKAFOR ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle pia imemwongeza mshambuliaji wa RB Salzburg ya Uswisi, Noah Okafor, 21, kwenye orodha ya wachezaji inaoweza kuwasajili mwezi huu. ***(Teamtalk)***

### GIVEN AMSHAURI KELLEHER

GOLIKIPA wa zamani wa Newcastle, Shay Given amemshauri mwenzake, Caoimhin Kelleher, 23, kuondoka Liverpool katika dirisha la uhamisho la Januari hii. ***(Premier Sport via Liverpool Echo)***

### MATETA KUONDOKA PALACE

MSHAMBULIAJI wa Crystal Palace, Jean-Philippe Mateta, 24, anakaribia kuondoka katika klabu hiyo mwezi huu, huku mshambuliaji huyo wa Ufaransa ambaye yuko kwa mkopo kutoka Mainz, akitarajiwa kuhamia kwa mkopo kwa St Etienne inayoshiriki Ligue 1. ***(Standard)***

### KOLASINAC KUTIMKA ARSENAL

MLINZI wa Arsenal, Sead Kolasinac, 28, amefanya mazungumzo na Marseille kuhusu uhamisho wa bila malipo msimu wa majira ya joto, huku beki huyo wa kushoto wa Bosnia akiwa hana nafasi kwenye Uwanja wa Emirates. ***(L'Equipe via Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BRUNO FERNANDES AIKATAA BARCELONA

**Asema mwaka mpya umeanza siku chache zilizopita, lakini tayari tumeshafika siku ya wajinga...**

**MANCHESTER,** England

BRUNO Fernandes alitania kuwa siku ya wajinga ya Aprili Mosi imekuja mapema wakati kiungo huyo wa Manchester United akikanusha uvumi wa kuhusishwa na mpango wa kuhamia Barcelona.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno anakaribia kutimiza miaka miwili tangu atue United akitokea Sporting CP na alikuwa anachukuliwa kama mmoja wa viungo bora zaidi wa klabu hiyo kwa wakati huo.

**Hata hivyo, ripoti kutoka nyumbani kwao na Fernandes zilibainisha kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anataka kuondoka hapo Old Trafford na amepewa ofa na Barcelona.**

Fernandes haraka alijibu ripoti hizo kupitia kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Mwaka mpya umeanza siku chache zilizopita, lakini tayari tumeshafika siku ya wajinga Aprili Mosi," alisema akinukuliwa na SPORT TV.

"Au hiyo ni sehemu ya uandishi mbaya?"

Fernandes bado ana miaka mitatu na nusu kwenye mkataba wake wa sasa ambao alisaini wakati akitua hapo Sporting kwa ada ya pauni milioni 68 Januari mwaka 2020.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
NIGERIA
VERSUS
EGYPT
1 | 3.02
X | 2.92
2 | 2.52

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOURINHO ASHANGAA KICHAPO



**ROME,** Italia

JOSE Mourinho amesema kikosi chake cha Roma kilipatwa na tatizo la kisaikolojia baada ya kuruhusu mabao matatu ndani ya dakika saba wakati wakifungwa na Juventus.

Roma walikuwa mbele kwa mabao 3-1 ndani ya dakika 20 kabla ya Juve kupindua meza.

Roma walipata penalti dakika za majeruhi iliyopigwa na Lorenzo Pellegrini, lakini ikaokolewa na Wojciech Szczesny baada ya Matthijs de Ligt kuonyeshwa kadi ya pili ya njano.

"Tulifanya vizuri sana ndani ya dakika 70, lakini baada ya hapo tulipata matatizo ya kisaikolojia," alisema Mourinho akiiambia DAZN.

"Wakati unapokuwa kwenye matatizo unatakiwa kuonyesha uwezo wako, lakini hatukuwa kwenye wakati huo."

# Arteta alalamikia kiwango Arsenal

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amelalamikia kiwango cha Arsenal kwenye kichapo cha bao 1-0 kwenye Kombe la FA kutoka kwa Nottingham Forest, akisema "hatukukaribia ubora uliotakiwa."

Kipigo hicho kinamaanisha kwamba, Arsenal wametolewa kwenye michuano hiyo raundi ya tatu.


Arteta alirudi kwenye benchi baada ya kulazimika kujitenga kutokana na maambukizi ya virusi vya corona ambapo alikosa kwenye mchezo wa kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Manchester City wikendi iliyopita.

Lakini hakuwa na furaha wakati bao la Lewis Grabban aliyetokea benchi lilipowapa ushindi Forest.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Arteta aliiambia ITV Sport: "Tupo nje ya mashindano na tunatakiwa kuomba radhi.

"Wakati ukiwa na wachezaji tisa nje, hilo ni pigo kubwa, lakini sitaki kutumia hicho kama kisingizio.

"Timu niliyoipanga nilitarajia ingecheza vizuri, lakini mambo yalikuwa tofauti na matarajio."



CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA



# NYOTA WA ZAMANI TATIZO PAMBA FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Pamba inayoshiriki Ligi ya Championship, ikipigania kupanda Ligi Kuu msimu ujao, imesema baadhi ya wachezaji waliowahi kuichezea timu hiyo kwa mafanikio makubwa, ndiyo wamekuwa chachu ya matatizo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya klabu hiyo, Alhaj Majogolo, amesema kutofanya vema kwa klabu hiyo kunatokana na misuguano ya ndani ya hapa na pale ambayo inaletwa na baadhi ya wachezaji nyota waliochezea timu hiyo wakati huo ikitwa 'Tout Puissant Lindanda', ambao wanaamini kuwa bila wao, basi wengine waliobaki hawawezi kuongoza.

Hii inatokana na malalamiko ya baadhi ya wachezaji wa zamani wa timu hiyo kudai kuwa viongozi hawana ushirikiano na wadau wa soka, pamoja na wao kutoa mawazo yao.

"Shida kubwa ni kila mmoja anafikiria anahitaji kuongoza Pamba, na vita ya nje ni kubwa mno. Kuna baadhi ya wachezaji wa zamani wa Pamba wanaisaidia sana timu hii kwa hali na mali, lakini baadhi yao wanaona kuwa wana uwezo wa kuongoza na wanaamini kama ni kocha lazima atoke miongoni mwao.

"Pia usajili wao ndiyo watafute wachezaji na hata viongozi wa kuiongoza klabu kama siyo wao, basi ni lazima uongozi utakaokuwa madarakani wao ndiyo wapendekeze," alisema Majogolo.

Alisema kuwa uongozi haujafunga milango na unapokea ushauri kutoka kwa mtu yeyote yule kwa ajili ya maendeleo ya Pamba FC.

Timu hiyo ambayo ilitwaa ubingwa wa Jamhuri wa Muungano mwaka 1990, inashika nafasi ya saba ikiwa na pointi 19 zilizotokana na mechi 14.



Mbunge wa Mtambile, Seif Salim Seif (kulia), akikabidhi kombe kwa nahodha wa timu ya Juhudi baada ya kushinda mashindao ya jimbo. Mbali ya kombe hilo, timu hiyo pia ilizawadiwa shilingi milioni moja. **NA MPIGAPICHA WETU**



# *Mbunge amwaga zawadi Jimbo Cup*

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MBUNGE wa Mtambile, Seif Salim Seif, amewazawadia washindi mbalimbali wa michuano ya mpira wa miguu ya jimboni mwake yaliyomalizika juzi kwenye Uwanja wa Kengeja, Pemba.

Mashindano hayo yalishirikisha jumla ya timu 20 ambapo timu ya Juhudi ilifanikiwa kutwaa ubingwa huo baada ya kuifunga timu ya Mizingani mabao 2-0.

Juhudi FC ilizawadiwa kombe pamoja na shilingi milioni moja, medali ya dhahabu na mipira 10 kutoka kwa mheshimiwa Seif ambaye ni Mbunge kupitia Chama Cha Wananchi (CUF).

Mbali ya kutwaa kombe, mchezaji Hafidhi Ali Maalim wa timu hiyo aliibuka na tuzo ya mchezaji bora wa mshindano na kiatu chenye thamani ya Sh.100,000.

Mheshimiwa Seif pia aliizawadia timu ya Mizingani Sh. 500,000, mipira mitano na jezi seti moja kwa kushika nafasi ya pili wakati mshindi wa tatu timu ya Maendeleo ikizawadiwa Sh. 300,000, jezi seti moja na mipira mitatu.

Kwa upande wa mshindi wa nne, timu ya Warriors ilizawadiwa Sh. 200,000, jezi seti moja na mipira miwili huku timu Mtadoda FC ikizawadiwa Sh. 250,000 na mipira miwili kwa kuwa timu yenye nidhamu.

Akizungumza wakati wa ufungaji wa mashindano hayo, Seif alisema mbali ya kuendeleza mpira wa miguu, mashindano hayo pia yana lengo la kudumisha umoja na kutafuta wachezaji wa kuunda timu ya jimbo lake ambayo itashiriki katika mashindano mbalimbali.

Alisema mpaka sasa amevutiwa na wachezaji wengi wenye vipaji ambao wanatakiwa kuendelezwa ili kufikia kiwango cha kuchezea timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars).

"Malengo yamefanikiwa kwani kupitia mashindano haya, tumeweza kuwa pamoja na kushikamana mbali ya kushindana kupitia timu zetu, nazipongeza timu shiriki, mashabiki na viongozi walioshiriki kufanikisha mashindano haya," alisema Seif.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 11/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1589 | Cardiff City U23 vs Ipswich U23 | 1.64 | 4.20 | 4.70 |
| 14:00 | 5410 | Vitoria Guimaraes U23 vs Sporting CP U23 | 2.65 | 3.33 | 2.36 |
| 15:40 | 3357 | AL Tai vs Al Hilal Riyadh | 7.00 | 4.50 | 1.44 |
| 16:00 | 1091 | Algeria vs Sierra Leone | 1.07 | 8.51 | 59.38 |
| 16:00 | 3971 | Sheffield United U23 vs Barnsley U23 | 1.41 | 4.52 | 5.97 |
| 16:00 | 4860 | Shabab AL Ahli Dubai Club vs AL Khaleej Khor Fakkan | 1.63 | 3.57 | 4.83 |
| 16:00 | 5795 | QPR U23 vs Bristol City U23 | 2.46 | 3.62 | 2.39 |
| 17:00 | 5118 | Jamshedpur vs East Bengal | 1.50 | 4.15 | 5.22 |
| 17:40 | 4197 | Al Salmiyah vs Kazma SC | 2.60 | 3.45 | 2.60 |
| 18:00 | 1550 | Benfica U23 vs Portimonense U23 | 1.45 | 4.24 | 5.79 |
| 18:05 | 4889 | Al Faisaly (KSA) vs Al Ahli Jeddah | 2.52 | 3.36 | 2.67 |
| 18:30 | 1493 | Jazira Abu Dhabi vs Al Wasl Dubai | 2.03 | 3.18 | 3.42 |
| 19:00 | 3433 | Nigeria vs Egypt | 3.02 | 2.92 | 2.52 |
| 19:55 | 4588 | Al Kuwait SC vs AL Arabi | 2.03 | 3.60 | 3.50 |
| 20:00 | 2641 | JS Kabylie vs US Biskra | 1.71 | 3.45 | 5.40 |
| 20:00 | 3434 | ASO Chlef vs JS Saoura | 4.00 | 2.85 | 2.17 |
| 20:00 | 3481 | MC Alger vs Paradou AC | 2.11 | 2.60 | 5.00 |
| 22:00 | 1284 | Sudan vs Guinea Bissau | 3.16 | 2.96 | 2.41 |
| 22:00 | 3159 | Arsenal U21 vs Chelsea U21 | 2.15 | 3.77 | 2.70 |
| 22:00 | 4731 | Cambridge Utd vs Portsmouth | 3.18 | 3.37 | 2.04 |
| 22:30 | 2738 | Mansfield vs Swindon Town | 2.55 | 3.38 | 2.55 |
| 22:45 | 1119 | Hayes Yeading United vs Weston Super Mare | 1.48 | 4.34 | 5.21 |
| 22:45 | 1360 | Warrenpoint vs Dungannon Swifts | 2.51 | 3.76 | 2.30 |
| 22:45 | 1421 | Kings Lynn vs Notts County | 6.00 | 4.70 | 1.46 |
| 22:45 | 1651 | Metropolitan Police vs Farnborough Town | 2.37 | 3.58 | 2.51 |
| 22:45 | 1799 | MK Dons vs AFC Wimbledon | 1.79 | 3.58 | 4.12 |
| 22:45 | 1837 | Southampton vs Brentford | 1.98 | 3.46 | 3.76 |
| 22:45 | 2044 | Cagliari vs Bologna | 2.85 | 3.35 | 2.44 |
| 22:45 | 2049 | Salford City vs Tranmere | 2.13 | 3.25 | 3.30 |
| 22:45 | 2088 | Scarborough Athletic vs Buxton FC | 3.27 | 3.61 | 1.93 |
| 22:45 | 2676 | Southend vs Yeovil | 2.78 | 3.27 | 2.39 |
| 22:45 | 3080 | Radcliffe Borough vs Bamber Bridge | 3.60 | 3.85 | 1.92 |
| 22:45 | 3134 | Kidderminster vs Farsley Celtic | 1.44 | 4.24 | 5.97 |
| 22:45 | 3219 | Stalybridge vs Atherton Collieries | 2.33 | 3.33 | 2.70 |
| 22:45 | 3313 | Potters Bar Town vs Margate | 2.50 | 3.66 | 2.34 |
| 22:45 | 3458 | Altrincham vs Stockport | 4.01 | 3.62 | 1.79 |
| 22:45 | 3716 | Forest Green vs Colchester | 1.57 | 3.83 | 5.50 |
| 22:45 | 4437 | Horsham vs Enfield Town | 2.60 | 3.76 | 2.23 |
| 22:45 | 4896 | Nantwich Town vs Gainsborough | 2.52 | 3.35 | 2.47 |
| 22:45 | 5086 | Tamworth vs Peterborough Sports | 2.84 | 3.61 | 2.13 |
| 22:45 | 5101 | Hyde United FC vs Matlock Town | 4.00 | 3.90 | 1.80 |
| 22:45 | 5146 | Brackley Town vs Kettering Town | 1.63 | 3.81 | 4.44 |
| 22:45 | 5209 | Sunderland vs Lincoln | 1.51 | 4.14 | 5.71 |
| 22:45 | 5272 | Ashton Utd vs Morpeth Town | 2.55 | 3.65 | 2.55 |
| 22:45 | 5364 | Halifax vs Grimsby | 1.72 | 3.67 | 4.31 |
| 22:45 | 5553 | Alvechurch vs Needham Market | 1.69 | 3.94 | 3.94 |
| 22:45 | 5860 | Boreham Wood vs Wealdstone | 1.66 | 3.71 | 4.69 |
| 22:45 | 5883 | Salisbury City vs Tiverton Town | 2.32 | 3.81 | 2.46 |
| 23:00 | 5052 | Reading vs Fulham | 4.89 | 4.10 | 1.58 |
| 23:00 | 5831 | Bolton vs Wycombe | 2.50 | 3.18 | 2.74 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Januari 11, 2022

Nipashe




Fernandes aikataa Barcelona UKURASA 21

# Azam yazima 'dabi' Simba, Yanga Z'bar

## ●●● Yassin Mustapha arudisha kombe rasmi, sasa...

**Na Adam Fungamwango**

NDOTO za watani wa jadi Simba na Yanga kukutana kwenye fainali ya Kombe la Mapinduzi kama ilivyokuwa mwaka jana, zimeyeyuka rasmi jana jioni kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar, baada ya Azam FC kutinga hatua ya fainali, ikiwachapa Wanajangwani hao kwa mikwaju ya penalti 9-8.

**Kwa matokeo hayo, Yanga imevuliwa rasmi ubingwa wa michuano hiyo na kuzima uwezekano wa 'dabi' nyingine kupigwa kwenye visiwa vya karafuu, kwani matokeo yoyote ya mechi ya jana usiku kati ya Simba dhidi ya Namungo hayabadili chochote.**

Penalti iliyoota mbawa ya beki Yassin Mustapha kwenye mechi hiyo ya nusu fainali, ndiyo iliwaondoa Yanga kwenye michuano hiyo na kuwasononesha mashabiki wa timu hiyo uwanjani hapo na wale waliokuwa wakifuatilia kwenye televisheni pamoja na wasikilizaji kwa njia ya redio.

Yassin, ndiye mchezaji pekee aliyekosa penalti hiyo, huku kukiwa hakuna hata kipa mmoja kati ya Mathias Kigonya wa Azam na Erick Johora ambaye aliingizwa dakika za majeruhi kwa ajili ya kazi ya kuokoa mikwaju huyo akichukua nafasi ya Aboutwalib Mshery, lakini alishindwa kufanya chochote, zaidi ya kushuhudia penalti zote tisa zikitinga wavuni.

Timu hizo zililazimika kupigiana penalti baada ya kutoka suluhu bila kufungana kwa dakika 90 za mchezo.

Wachezaji waliokwamisha mipira wavuni kwa upande wa washindi ni Lusajo Mwaikenda, Rodgas Kola, Kenneth Muguna, Yahya Zaid, Aggrey Morris, Daniel Amoah, Tepsi Evance, Paul Katema, huku Mudathir Yahaya akienda kufunga penalti ya mwisho, baada ya Yassin wa Yanga kukosa.

Kwa upande wa Yanga, walioweka mpira nyavuni ni Jesus Moloko, Zawadi Mauya, Dickson Job, Fiston Mayele, Saido Ntibazonkiza, Yannick Bangala, Dickson Ambundo na Farid Mussa, kabla ya mkosaji kwenda kupiga.

Ilionekana kabisa kipindi cha pili Azam kuhitaji zaidi kwenda kwenye mikwaju ya penalti, kwani ilikuwa ikizuia zaidi na kukaa na mpira wakiwa wamejazana katikati, wakiacha straika mmoja mbele, huku Yanga wakionekana kuchoka kadri muda ulivyozidi kusonge mbele.

Mechi ilianza kwa timu zote kuanza kushambuliana kwa zamu, huku soka likiwa la wazi kuliko kipindi cha pili.

Faulo ya Ibrahim Ajibu dakika ya nne ya mchezo, nusura izae bao, baada ya Aggrey Morris kupiga kichwa kilichotoka juu kidogo ya lango la Yanga.

Yanga ilijibu shambulio hilo dakika tatu baadaye, wakati Heritier Makambo alipoingia ndani ya eneo la hatari la Azam, baada ya pande kutoka kwa Ntibazonkiza, lakini shuti lake la mguu wa kushoto lilitoka sentimeta chache nje ya lango.

Yanga ilionekana sasa imehamia kwenye lango la Azam, kwani dakika ya 12, Ntibazonkiza aliupata mpira uliokuwa ukizagaa kwenye eneo la Azam, akapiga shuti kali ambalo lilidakwa kwa ustadi na kipa Mathias Kigonya.

Ikawa zamu ya Azam nayo iliweka majaribuni lango la wapinzani wao, kwani ilikaribia kuandika bao dakika ya 26, kama si shuti la Ismail Aziz aliyekuwa ndani ya eneo la hatari kutoka nje kidogo ya lango.

Dakika tatu baadaye, Ajibu alipiga shuti la mbali, kiasi cha mita 35 ambalo lingeweza kuwa la hatari kama lingelenga lango, kwani kipa Mshery alikuwa ameshapotea.

MILIKI...



Winga wa Azam FC, Tepsi Evance, akimiliki mpira dhidi ya kiungo wa Yanga, Yanick Bangala kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa Uwanja wa Amaan, Zanzibar jana na Azam kushinda kwa penalti 9-8 baada ya timu hizo kutoka suluhu ndani ya dakika 90. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Simba na 'sapraizi' usajili bab'kubwa

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

ACHANA na matokeo ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi jana dhidi ya Namungo FC, habari ya mjini ni 'sapraizi' bab'kubwa ambayo uongozi wa Klabu ya Simba utaitoa kwa mashabiki wa timu hiyo katika dirisha hili dogo la usajili, imeelezwa.

Simba ambao ni mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu minne mfululizo ikiwa nafasi ya pili na pointi 24 baada ya kucheza mechi 10, nyuma ya Yanga inayoongoza msimamo kwa alama 29, lakini yenyewe ikicheza mechi 11, jana usiku ilivaana na Namungo katika Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar.

Katika michuano hiyo ya Mapinduzi kuna wachezaji watatu wanafanya majaribio Simba, kiungo mkabaji kutoka Nigeria Udoh Etop David, winga Cheick Moukoro kutoka Ivory Coast na nyota wa zamani wa timu hiyo, Msudan Sharaf Eldin Shaiboub Ali.

Hata hivyo, licha ya mashabiki wa Simba kuonekana kuvutiwa zaidi na Udoh Etop licha ya kupata dakika chache uwanjani dhidi ya Mlandege Ijumaa iliyopita, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco, alisema anahitaji muda kumtazama tena katika mchezo wa jana kabla ya kutoa mapendekezo yake nani asajiliwe kati ya nyota hao watatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Idara ya Habari ya klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema mashabiki na wanachama, watulie na viongozi wapo kazini kuhakikisha timu yao inasukwa na kurejea na moto mkali kwenye mechi za Ligi Kuu.

Alisema baada ya michuano hiyo kila kitu kitawekwa wazi ikiwa ni pamoja na usajili watakaoufanya huku akieleza ugumu wanaoupata kwenye Ligi Kuu ni kutokana na kukamiwa na timu pinzani, kadri siku zinavyosonga mbele, lakini mambo yatakuwa mazuri na kufikia malengo yao.

"Tutafanya vizuri michezo ijayo, msimu uliopita ilikuwa hivi, waliongoza ligi hatimaye tukachukuwa ubingwa, nina imani msimu huu tutafanya vizuri tu," alisema.

Alisema viongozi wakishirikiana na benchi la ufundi la timu hiyo chini ya Kocha Mkuu, Pablo Franco wamejipanga kuhakikisha wanarudi kwenye ligi wakiwa na moto, wakitimiza pia malengo yao kwa msimu huu katika michuano ya kimataifa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >